Maelezo ya

# Nyakati saba za kanisa

## Sura ya Tano

## Wakati wa Kanisa la Pergamo

Ufunuo 2:12-17

*Na kwa malaika wa kanisa lililoko Pergamo andika; Haya ndiyo anenayo Yeye aliye na huo upanga mkali, wenye makali kuwili.*

*Nayajua matendo yako, na mahali ukaapo, ndipo penye kiti cha enzi cha Shetani; nawe walishika sana Jina Langu, wala hukuikana imani Yangu, hata katika siku za Antipa shahidi Wangu, mwaminifu Wangu, aliyeuawa kati yenu, hapo akaapo Shetani.*

*Lakini ninayo maneno machache juu yako, kwa kuwa unao huko watu washikao mafundisho ya Balaamu, yeye aliyemfundisha Balaki atie ukwazo mbele ya Waisraeli, kwamba wavile vitu vilvyotolewa sadaka kwa sanamu, na kuzini.*

*Vivyo hivyo wewe nawe unao watu wayashikao mafundisho ya Wanikolai, ambayo Mimi nayachukia.*

*Basi tubu; na usipotubu, naja kwako upesi, nami nitafanya vita juu yao kwa huo upanga wa kinywa Changu.*

*Yeye aliye na sikio na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa. Yeye ashindaye nitampa baadhi ya ile mana iliyofichwa, nami nitampa jiwe jeupe, na juu ya jiwe hilo limeandikwa jina jipya asilolijua mtu ila yeye anayelipokea.*

**PERGAMO**

Pergamo (jina la kale) lilikuwa Mysia, katika wilaya iliyotiwa maji na mito mitatu, ambapo mmoja wao uliwezesha kuwasiliana na bahari. Ulielezewa kama mji uliokuwa maarufu kuliko yote katika Asia. Ulikuwa mji wa utamaduni na wenye maktaba ya pili kwa ukubwa kutoka ile iliyokuwa Aleksadria. Hata hivyo ulikuwa ni mji wenye dhambi nyingi, uliopenda sana ibada za uasherati za Eskalpia, ambaye walimwabudu katika mfano wa nyoka aliye hai aliyewekwa na kulishwa hekaluni. Katika mji huu mzuri wenye vichaka vilivyonyweshewa maji, barabara na bustani, kuliishi kundi dogo la Wakristo waliojiweka wakfu ambao hawakupumbazwa na uzuri wa nje, na walichukia ibada za Shetani zilizojaa mahali pale.

**MUDA WENYEWE**

Wakati wa Pergamo ulidumu yapata miaka mia tatu, kutoka 312 hadi 606 A.D.

**MJUMBE**

Tukitumia kanuni yetu tuliyopewa na Mungu ya kumchagua mjumbe kwa kila wakati, hiyo ni kusema, tunamchagua yule ambaye huduma yake inakaribia sana ile ya mjumbe wa kwanza, Paulo, tunatangaza bila kusita mjumbe wa Pergamo kuwa ni Martin. Martin alizaliwa mwaka wa 315 huko Hungary. Walakin, kazi ya maisha yake ilikuwa huko Ufaransa ambako alitumika hapo Tours na kandokando yake kama askofu. Alikufa mnamo mwaka wa 399. Mtakatifu huyu mashuhuri alikuwa ni mjomba wa Mkristo mwingine wa ajabu, Mtakatifu Patrick wa Ireland.

Martin aliongoka kwa Kristo wakati alipokuwa akifanya kazi ya askari wa kulipwa. Ilikuwa katika kipindi alipokuwa angali anafanya kazi hii ambapo muujiza wa ajabu sana ulitukia. Imeandikwa ya kwamba maskini mmoja alikuwa mgonjwa amekaa kwenye barabara za mji mahali Martini alipokuwa ametumwa kazini. Baridi ya majira ya kipupwe ilikuwa zaidi ya vile angeweza kuvumilia kwa kuwa hakuwa na nguo za kutosha. Hakuna mtu aliyejali mahitaji yake mpaka Martin alipopita. Alipoona hali mbaya ya mtu huyu maskini, lakini akiwa hana nguo nyingine ya ziada, alivua koti lake la baridi, akalikata vipande viwili kwa upanga wake, kisha akamsetiri kwa vazi hilo huyo mtu aliyekuwa anakufa kwa baridi. Alimhudumia kadiri alivyoweza na akaenda zake. Usiku huo Bwana Yesu alimtokea katika ono. Hapo Yeye alisimama, kama mwombaji, amevikwa nusu ya vazi la Martin. Akanena naye akamwambia, “Martin, ingawa yeye ni mwanafunzi wa katekisimo tu amenivika nguo Mimi kwa vazi hili.” Tangu wakati huo na kuendelea Martin alijaribu kumtumikia Bwana kwa moyo wake wote. Maisha Yake yakawa mfululizo wa miujiza ikidhihirisha nguvu za Mungu.

Baada ya kuondoka jeshini na kuwa kiongozi kanisani, alichukua msimamo mkali sana dhidi ya ibada za sanamu. Akakatakata maashera, akavunja sanamu na kuzibomoa madhabahu. Alipokabiliwa na wapagani kwa ajili ya vitendo vyake yeye alishindana nao kwa kadiri ya namna ile ile Eliya aliyoshindana

na manabii wa Baali. Alijitolea kufungwa kwenye mti upande wake wa chini ili kwamba wakati utakapokatwa ungemponda isipokuwa Mungu aliingilia kati na kuugeuza ule mti wakati ulipoanguka. Hao makafiri wenye hila wakamfunga kwenye mti uliokuwa unakua kwenye mtelemko wa kilima, wakiwa na uhakika ya kwamba mvuto wa kawaida wa nguvu za uvutano wa dunia ungeufanya huo mti kuanguka hivi kwamba ungemponda-ponda. Mara mti huo ulipoanza kuanguka, Mungu aliugeuza kuelekea upande wa juu wa kile kilima, kinyume cha tabia zote za maumbile. Wale makafiri waliokuwa wanakimbia walipondwa-pondwa wakati huo mti ulipowaangukia wengi wao.

Wanahistoria wamekiri ya kwamba katika mara zisizopungua tatu alifufua wafu kwa imani katika Jina la Yesu. Katika tukio moja alimwombea mtoto mchanga aliyekuwa amekufa. Kama Elisha, alijinyosha juu ya mtoto mchanga na kuomba. Alifufuka akawa hai na mwenye afya. Katika tukio jingine aliitwa akasaidie kumwokoa ndugu mmoja aliyekuwa amechukuliwa akauawe wakati wa mateso makuu. Wakati alipofika maskini huyo alikuwa tayari amekufa. Walikuwa wamemtundika mtini. Mwili wake haukuwa na uhai na macho yake yalikuwa yametokeza kutoka kwenye soketi za macho. Lakini Martin alimshusha chini, na wakati alipokwisha kuomba huyo mtu akafufuka na kupewa jamaa yake iliyojaa furaha.

Martin kamwe hakumwogopa adui haidhuru alikuwa ni nani. Hivyo basi alienda mwenyewe binafsi kumkabili mfalme mkatili ambaye alikuwa amehusika na vifo vya watakatifu wengi waliojazwa Roho. Huyo mfalme hakukubali kuzungumza naye, kwa hiyo Martin akaenda kumwona rafiki wa huyo mfalme, mtu mmoja jina lake Damasus, askofu katili wa Rumi. Lakini askofu huyo, akiwa Mkristo wa jina tu wa ule mzabibu wa uongo alikataa kumtetea. Martin akarudi kwenye jumba la mfalme, lakini hadi kufikia wakati huo milango ilikuwa imekwisha fungwa nao hawakumkubalia kuingia. Alilala kifudifudi mbele za Bwana na akaomba apate kuingia kwenye jumba la mfalme. Akasikia sauti ikimwambia ainuke. Alipoinuka, aliona milango ikijifungua yenyewe. Akaenda akaingia barazani. Lakini huyo mtawala mwenye majivuno hakugeuza kichwa chake na aseme naye. Martin aliomba tena. Mara moto ukatokea wenyewe kutoka kwenye kile kiti cha mfalme na mfalme huyo mshari akaondoka kitini mbio. Hakika Bwana huwadhili wenye kiburi na kuwainua wanyenyekevu.

Hiyo ilikuwa ndiyo bidii yake katika kumtumikia Bwana hata Ibilisi aliamshwa kwa nguvu. Maadui wa ile kweli waliwaajiri wauaji ili wamwue Martin. Wakaja kwa kunyemelea nyumbani kwake na walipokuwa wanataka kumwua, alisimama wima na kutoa shingo yake ikatwe kwa upanga. Walipokuwa wanaruka mbele, mara nguvu za Mungu zikawatupa nyuma kwa nguvu mpaka upande wa pili wa kile chumba. Walishindwa sana katika mazingara hayo matakatifu na ya kuogofya hivi kwamba walitambaa kwa mikono yao na magoti yao na kuomba msamaha kwa kujaribu kumwua.

Mara nyingi sana wakati watu wanapotumiwa sana na Bwana wanajiinua kwa majivuno. Lakini sivyo ilivyo kwa Martin. Yeye daima alidumu mtumishi mnyenyekevu wa Mungu. Usiku mmoja alipokuwa anajitayarisha kwenda mimbarani, maskini mmoja alikuja kwenye chumba chake cha kujisomea akaomba nguo. Martin alimpeleka yule ombaomba kwa shemasi wake mkuu. Yule shemasi mwenye kiburi akamwamuru aondoke. Hapo akarudi kumwona Martin. Martin akaondoka na kumpa mwombaji joho lake zuri, akamwambia shemasi amletee joho lingine ambalo lilikuwa la kiwango duni. Usiku huo wakati Martin alipokuwa anahubiri Neno, kundi la Mungu liliona nuru nyeupe ya kupendeza inayomeka ikimzunguka.

Hakika huyu alikuwa ni mtu mashuhuri, mjumbe wa kweli kwa wakati huo. Kamwe hakutaka cho chote ila kumpendeza Mungu aliishi maisha yaliyowekwa wakfu sana. Kamwe hangeweza kushawishiwa kuhubiri mpaka kwanza ameomba na yuko katika hali nzuri ya kiroho kujua na kuleta mausia yote ya Mungu kwa Roho Mtakatifu aliyetumwa kutoka mbinguni. Mara nyingi angewaweka watu wangoje huku anaomba apate hakikisho kamili.

Kujua tu habari za Martin na huduma yake kuu kunaweza kumfanya mtu awazie ya kwamba mateso ya watakatifu yalikuwa yamepungua. Sivyo. Bado walikuwa wangali wanaangamizwa na ibilisi kwa njia ya watu wakatili. Walichomwa moto. Walipigiliwa misumari kwenye magogo uso ukielekea chini na mbwa wakali waliachiliwa wawashambulie, hivi kwamba hao mbwa wangewachana nyama ya mwili na matumbo, wakiwaacha waliopatwa na hayo kufa katika uchungu mkuu. Watoto wachanga walitolewa kwenye matumbo ya mama waja wazito na kutupiwa nguruwe mwitu. Matiti ya wanawake yalikatwa, na walilazimishwa kusimama wima huku kila pigo la moyo lilimwaga damu mpaka wakaanguka chini wakafa. Na msiba huo ulikuwa mkuu hata na zaidi kuuwazia wakati mtu anapotambua ya kwamba hivi havikuwa ni vitendo tu vya makafiri, lakini mara nyingi vilisababishwa na hao, wanaosemekana kuwa ni waliojiita Wakristo waliojisikia kwamba walimtetea Mungu katika kuwaangamiza askari hawa waaminifu wa msalaba waliolitetea Neno na kumtii Roho Mtakatifu.

Yohana 16:2,

*"Watawatenga na masinagogi; naam, saa yaja atakapodhania kila mtu awauaye ya kuwa anamtolea Mungu ibada."*

Mathayo 24:9,

*"Wakati huo watawasaliti ninyi mpate dhiki, nao watawaua; nanyi mtakuwa watu wa kuchukiwa na mataifa yote kwa ajili ya Jina Langu."*

Kwa ishara na maajabu, kwa nguvu za Roho, Martin kweli alithibitishwa kama mjumbe wa wakati huo. Lakini si kwamba tu yeye alikirimiwa huduma kuu, yeye mwenyewe alikuwa mwaminifu daima kwa Neno la Mungu. Alipiga vita madhehebu. Alikemea dhambi mahali pa juu. Alitetea kweli kwa maneno na matendo na kuishi maisha kamili ya ushindi wa Kikristo.

Mwandishi wa habari za maisha yake aliandika juu yake hivi. "Hapana mtu aliyepata kumwona amekasirika, au kuwa na wasiwasi, au akihuzunika, au akicheka. Yeye daima alikuwa vile vile, na alionekana kama kitu ambacho ni zaidi ya mwanadamu, usoni mwake kukiweko na namna fulani ya furaha ya kimbinguni. Kamwe hapakuwa na cho chote kinywani mwake ila Kristo, hakukuwa na cho chote moyoni mwake ila uchaji, amani na huruma. Mara nyingi alililia dhambi hata na za wale wapinzani wake, ambao wakati alipokuwa amenyamaza na hayuko walimshambulia kwa midomo kama ya nyoka na ndimi zenye sumu. Wengi walimchukia kwa ajili ya nguvu ambazo wao wenyewe hawakuwa nazo na wala hawakuweza kuiga, na ole! maadui zake wabaya sana walikuwa ni maaskofu."

**SALAMU**

Ufunuo 2:12b

*"Haya ndiyo anenayo yeye aliye na huo upanga mkali, wenye makali kuwili."*

Ujumbe kwa wakati wa tatu wa kanisa uko karibu kutokea. Onesho la tatu la mchezo huu wa kuigiza wa "Kristo kati ya kanisa Lake" liko karibu kufunuliwa. Kwa sauti kama ya baragumu, Roho anamwonyesha Huyu Mweza Yote, "Yeye Aliye na huo upanga mkali wenye makali kuwili!" Jinsi onyesho hili lilivyo tofauti sana na wakati ambapo Pilato alivyomjulisha Mwana-Kondoo wa Mungu, amevikwa mavazi ya zambarau ya mzaha, amepigwa na kuvikwa taji ya miiba, akisema, "Mtazameni Mfalme wenu!" Sasa huku amevaa mavazi ya kifalme na kutiwa taji ya utukufu anasimama Bwana wetu aliyefufuka, „Kristo, nguvu za Mungu".

Katika maneno haya, 'Yeye aliye na upanga mkali wenye makali mawili' kuna ufunuo mwingine wa Uungu. Katika Wakati wa Efeso, mtakumbuka, Yeye alidhihirishwa kama Mungu asiyebadilika. Katika Wakati wa Smirna tulimwona kama Mungu MMOJA WA KWELI na kando Yake hakukuwa na mwingine. Sasa katika wakati huu wa Pergamo kuna ufunuo zaidi wa Uungu Wake, uliowekwa na ushirika Wake na ule upanga mkali wenye makali kuwili, ambao ni Neno la Mungu.

Waebrania 4:12

*"Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo."*

Waefeso 6:17

*"Tena upokeeni upanga wa Roho ambao ni Neno la Mungu."*

Ufunuo 19:13 & 15a,

*"Naye amevikwa vazi lililochovywa katika damu, na Jina Lake aitwa, Neno la Mungu. Na upanga mkali hutoka kinywani Mwake."*

Yohana 1:1-3,

*"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Huyo (Neno) mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa Huyo; wala pasipo Yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika."*

I Yohana 5:7,

*"Kwa maana wako watatu washuhudiao Mbinguni, Baba, na Neno, na Roho Mtakatifu, na watatu hawa ni MMOJA."*

Sasa tunaweza kuona ushirika Wake na Neno. YEYE NI NENO. Hilo ndilo Yeye alilo. NENO KATIKA JINA LAKE.

Katika Yohana 1:1 ambapo inasema *"Hapo mwanzo kulikuweko Neno,"* shina ambamo tunapata tafsiri yetu ya „Neno" ni „Logos" ambalo maana yake ni „wazo ama fikira." Lina maana maradufu ya „wazo" na „maneno". Sasa, wazo lililotamkwa ni "neno", au maneno. Je! hilo si ni la ajabu na zuri? Yohana anasema wazo la Mungu lilidhihirishwa katika Yesu.

Na Paulo anasema jambo lile lile katika Waebrania 1:1-3,

> *"Mungu, Ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi,*
>
> *Mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana (Logos), aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa Yeye aliufanya ulimwengu;*
>
> *Yeye kwa kuwa ni mng"ao wa utukufu Wake na chapa ya nafsi Yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza Wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi zetu, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu."*

Mungu alidhihirishwa katika utu wa Yesu Kristo. Yesu alikuwa Sura ya Nafsi ya Mungu.

Tena katika Yohana 1:14,

> *"Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu."*

*Nafsi Yenyewe ya Mungu ilifanyika mwili ikakaa kwetu.* Yule Mungu-Roho aliye mkuu ambaye hakuna mtu angeweza kumkaribia, Ambaye hakuna mtu alikuwa amemwona wala angeweza kumtazama sasa alikuwa amefanya maskani Yake katika mwili na kukaa kati ya wanadamu, akidhihirisha ukamilifu wa Mungu kwa wanadamu.

Yohana 1:18,

> *"Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, Huyu ndiye aliyemfunua."*

Mungu, Ambaye mara kwa mara angedhihirisha uwepo Wake kwa wingu ama nguzo ya moto iliyoleta hofu mioyoni mwa watu; Mungu huyu, Ambaye tabia za moyo Wake zilidhihirishwa kwa ufunuo wa maneno tu kupitia kwa manabii, sasa akawa Imanueli (Mungu pamoja nasi) akijifunua Mwenyewe. Neno, „kufunua," linatolewa kwenye shina la Kiyunani ambalo mara nyingi tutalifasiri kama mafafanuzi, ambalo linamaanisha kueleza kinaganaga na kufanya dhahiri. Hivyo ndivyo NENO lililo Hai, Yesu, alivyofanya. Yeye alimleta Mungu kwetu, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Mungu.

Alitufunulia Mungu kwa uwazi mkamilifu sana ambao Yohana angeweza kusema kumhusu Yeye katika I Yohana 1:1-3

> *"Lile lililokuwako tangu mwanzo, tulilolisikia, (Logos maana yake ni maneno) tuliloliona kwa macho yetu, tulilolitazama, na mikono yetu ikalipapasa, kwa habari ya Neno la Uzima;*
>
> *(Na Uzima huo ulidhihirika, nasi tumeuona, tena twashuhudia, na kuwahubiri ninyi ule Uzima wa Milele, uliokuwa kwa Baba, ukadhihirika kwetu);*
>
> *Hilo tuliloliona na kulisikia, twawahubiri na ninyi; ili nanyi pia mpate kushirikiana nasi; na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana Wake Yesu Kristo."*

Wakati Mungu alipofunuliwa kweli, Yeye alidhihirishwa katika mwili. *"Yeye aliyeniona Mimi amemwona Baba."*

Sasa turudi kwenye Ebr. 1:1-3 tuliona kwamba Yesu alikuwa ni sura ya nafsi ya Mungu. Alikuwa ni Mungu akijidhihirisha Mwenyewe katika mwanadamu kwa mwanadamu. Lakini kuna jambo jingine la kuangalia katika aya hizi, hasa aya ya kwanza na ya pili.

> *"Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwanawe."*

Ninawatakeni mwone hapa pambizoni mwa Biblia yako mtaona masahihisho. Neno, 'kwa' si tafsiri sahihi. Linapaswa kusema „NDANI YA". Si "kwa." Ndipo linasema kwa usahihi, "Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu NDANI YA manabii kwa njia ya Neno".

I Samweli 3:21b,

> *"Kwa kuwa Bwana akajifunua kwa Samweli huko Shilo, kwa Neno la Bwana."*

Hilo linaelezea I Yohana 5:7 kikamilifu, "Roho na Neno ni MMOJA." Yesu alimfunua Baba. Neno lilimfunua Baba. Yesu alikuwa Neno lililo Hai. Mungu asifiwe, leo Yeye angali ni Neno lile lililo Hai.

Wakati Yesu alipokuwa duniani alisema,

> *"Husadiki ya kwamba Mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani Yangu? Hayo Maneno niwaambiayo Mimi, siyasemi kwa shauri Langu; lakini ni Baba akaaye ndani Yangu huzifanya*

*kazi Zake."* Yn. 14:10.

Hapa inaelezwa dhahiri sana kwamba dhihirisho kamilifu la Mungu katika Mwana lilikuwa kwa Roho aliyekuwa akiishi ndani Yake akijidhihirisha katika Neno na kazi. Hilo ndilo hasa tumekuwa tukifundisha wakati wote. Wakati bibi-arusi atakaporudi kuwa bibi-arusi Neno, atafanya kazi zile hasa alizofanya Yesu. Neno ni Mungu. Roho ni Mungu. Wote ni MMOJA. Mmoja hawezi kutenda kazi bila huyo mwingine. Kama mtu kweli ana Roho wa Mungu, atakuwa na Neno la Mungu. Hivyo ndivyo ilivyokuwa na manabii. Walikuwa na Roho wa Mungu aliyekuwa akikaa ndani yao nalo Neno likawajilia. Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa Yesu. Ndani Yake mlikuwamo Roho bila kipimo na Neno lilimjia. (Yesu alianza kutenda na kufundisha. Mafundisho yangu si Yangu mwenyewe, bali ni ya Baba aliyenipeleka. (Matendo 1:1, Yohana 7:16.)

Kumbuka sasa, Yohana Mbatizaji alikuwa ni nabii na mjumbe wa siku yake. Yeye alijazwa na Roho Mtakatifu tangu tumboni mwa mama yake. Alipokuwa akibatiza katika Yordani Neno la Mungu (Yesu) lilimjia. Neno daima huwajia waliojazwa na Roho kweli. Huo ndio ushahidi wa kujazwa na Roho Mtakatifu. Hilo ndilo Yesu alilosema lingekuwa ushahidi. Yeye alisema, "Nami nitamwomba Baba Naye atawatumia Mfariji mwingine apate kukaa nanyi milele. Hata Roho wa kweli, ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea." Sasa tunajua Kweli ni nini.

*"Neno Lako ni Kweli."* (Yohana 17:17b)

Tena katika Yohana 8:43,

*"Mbona hamyafahamu hayo niyasemayo? Ni kwa sababu ninyi hamwezi kulisikia Neno Langu."*

Je! Uliona ya kwamba Yesu alisema ya kwamba ulimwengu usingeweza kumpokea Roho Mtakatifu? Vema, katika aya hii niliyosoma hivi punde, wala hawangeweza kulipokea Neno. Kwa nini? Kwa sababu Roho na Neno ni mmoja, na kama una Roho Mtakatifu kama wale manabii, Neno halina budi kuja kwako. Ungelilipokea.

Katika Yohana 14:26,

*"Lakini huyo Msaidizi. Huyo Roho Mtakatifu, Ambaye Baba atampeleka kwa Jina Langu, ATAWAFUNDISHA yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia."*

Hapa tena tunaona Neno likija kwa sababu ya Roho wa Mungu.

Tena katika Yohana 16:13

*"Lakini Yeye atakapokuja, huyo Roho wa Kweli (Neno), atawaongoza awatie kwenye kweli yote (Neno Lako ni kweli); kwa maana hatanena kwa shauri Lake Mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia (Neno la Mungu) atayanena (Neno), na mambo yajayo atawapasha habari yake."(Roho akileta Neno la Unabii).*

Ninawataka muangalie kwa makini sana ya kwamba Yesu hakusema ya kwamba ushuhuda wa kubatizwa na Roho Mtakatifu ulikuwa ni kunena kwa lugha, kufasiri, kutoa unabii, au kupiga makele na kucheza. Alisema ushuhuda ungekuwa ya kwamba wewe utakuwa katika KWELI; utakuwa katika Neno la Mungu kwa wakati wako. Ushahidi unahusiana na kupokea Neno hilo.

Katika I Wakorintho 14:37,

*"Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana."*

Sasa angalia jambo hilo. Thibitisho la Roho akaaye ndani ya mtu lilikuwa ni kukubali na KUFUATA yale nabii wa Mungu aliyotangazia huo wakati wake akiliweka kanisa kwenye utaratibu. Ilimbidi Paulo kuwaambia wale waliodai ufunuo mwingine, (aya yaa 36)

*"Au je! Neno la Mungu lilitoka kwenu? au kuwafikia ninyi peke yenu?"*

Ushuhuda wa Mkristo mwamini aliyejazwa na Roho si kuinena kweli (Neno), bali kupokea kweli (Neno), na kuliamini na kulitii.

Umeona katika Ufunuo 22:17

*"Na Roho na bibi-arusi wasema, Njoo! Naye asikiaye na aseme, Njoo!"*

Mnaona, bibi-arusi ananena Neno lile lile analonena Roho. Yeye ni bibi-arusi Neno akithibitisha yeye anaye Roho. Katika kila wakati wa kanisa tunasikia maneno haya,

*"Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa."*

Roho anatangaza Neno. Kama una Roho utalisikia Neno la wakati wako, kama vile wale Wakristo wa kweli walivyolichukua Neno kwa ajili ya wakati wao.

Je! Ulipata wazo hilo la mwisho? Ninarudia, kila wakati wa kanisa huishia kwa onyo lile lile. *"Yeye aliye na sikio, na alisikie (mtu binafsi) Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa."* Roho hutangaza Neno. Yeye ana kweli kwa kila wakati. Kila wakati umekuwa na wateule wake wenyewe, na kundi hilo teule daima „lilisikia neno," na kulipokea, ikithibitisha wao walikuwa na ile Mbegu ndani yao.

Yohana 8:47,

> *"Yeye aliye wa Mungu huyasikia maneno ya Mungu; hivyo ninyi hamyasikii kwa sababu ninyi si wa Mungu."*

Wao walilikataa Neno (Yesu) na Maneno Yake kwa siku zao, lakini uzao wa kweli ulilipokea Neno kwa sababu wao walikuwa ni wa Mungu.

> *"Na watoto Wako WOTE watafundishwa na Mungu."*

Isaya 54:13.

Yesu alisema jambo lile lile katika Yohana 6:45. Kuwa MMOJA NA NENO kunathibitisha kama wewe ni wa Mungu na umejazwa na Roho. Hakuna kigezo kingine.

Lakini lugha ni nini na kufasiri na karama nyingine? Hizo ni madhihirisho. Hivyo ndivyo Neno linavyofundisha.

Soma katika I Wakorintho 12:7,

> *"Lakini kila mmoja hupewa UFUNUO wa Roho kwa kufaidiana."*

Ndipo Paulo anataja madhihirisho hayo.

Sasa linakuja swali hili zuri sana ninalojua nyote mnataka sana kuuliza. Kwa nini madhihirisho si ushuhuda wa kubatizwa na Roho Mtakatifu, kwa sababu hakika hungeweza kumdhihirisha Roho Mtakatifu isipokuwa iwe ulikuwa umejazwa kweli na Roho? Sasa laiti ningaliweza kusema ya kwamba jambo hilo ni kweli, kwa sababu sipendi kuwaudhi watu ama kuyapuuza mafundisho yao; lakini nisingekuwa mtumishi wa kweli wa Mungu kama sikuwaambia shauri lote la Mungu. Hiyo ni kweli, sivyo?

Hebu tu tumwangalie kidogo Balaamu. Alikuwa wa kidini, alimwabudu Mungu. Alifahamu njia sahihi ya kutoa dhabihu na kumkaribia Mungu, lakini hakuwa nabii wa Uzao wa Kweli kwa maana alichukua ujira usio wa haki, na jambo baya sana kuliko yote aliwaongoza watu wa Mungu akawaingiza katika dhambi za uasherati na ibada za sanamu. Lakini ni nani angethubutu kukana ya kwamba Roho wa Mungu alijidhihirisha kupitia kwake katika moja ya sehemu nzuri sana za unabii ulio sahihi kabisa ulimwengu uliopata kuona? Lakini yeye kamwe hakuwa amepata Roho Mtakatifu.

Sasa basi, unafikirije juu ya Kayafa, yule kuhani mkuu? Biblia ilisema ya kwamba yeye alitabiri namna ya kifo ambacho Bwana atakufa. Sote tunajua hakuna taarifa yake ya kuwa mtu aliyejazwa na kuongozwa na Roho kama mzee mpendwa Simeoni ama yule mtakatifu mzuri sana aliyeitwa Ana. Hata hivyo alikuwa na dhihirisho halisi la Roho Mtakatifu. Hatuwezi kukana jambo hilo. Basi ni wapi ambapo dhihirisho ni kama ushuhuda? Hakuna. Kama wewe kweli umejazwa na Roho wa Mungu utakuwa na thibitisho la NENO maishani mwako.

Hebu niwaonyeshe kwa kina jinsi ninavyojisikia na kuufahamu ukweli huu kwa ufunuo alionipa Mungu. Sasa kabla sijawaambia, nataka kusema jambo hili. Wengi wenu ninyi watu mnaniamini mimi kuwa nabii. Sisemi ya kwamba ndivyo nilivyo. Ninyi ndio mliosema. Lakini sote tunajua ya kwamba maono anayonipa Mungu HAYASHINDWI KUTIMIA. HATA MARA MOJA. Kama mtu ye yote anaweza kuthibitisha ya kwamba ono lilipata kushindwa wakati wo wote nataka kujua kuhusu hilo. Sasa kwa sababu mmenifuata umbali huu, nawaleteeni kisa changu.

Miaka mingi iliyopita nilipokutana na Wapentekoste kwa mara ya kwanza, nilikuwa katika moja ya mikutano yao ya kambi ambapo kulikuwa na dhihirisho kubwa la lugha, tafsiri ya lugha, na unabii. Wahubiri wawili hasa walihusika katika namna hii ya kunena zaidi kuliko ndugu wengine wote. Niliifurahia sana ibada hiyo na kweli nilikuwa na nafurahia madhihirisho mbalimbali, kwa kuwa yalikuwa na ukweli halisi kwao. Nilitaka sana kujua yote niliyoweza kuhusu karama hizi, kwa hiyo nikaamua kuzungumza na hao watu wawili juu yake. Kupitia karama ya Mungu iliyo ndani yangu, nilitafuta kujua roho iliyokuwa ndani ya mtu wa kwanza, kama alikuwa wa Mungu kweli ama sivyo. Baada ya mazungumzo mafupi na yule ndugu mwema, mnyenyekevu, nilijua ya kwamba alikuwa ni Mkristo halisi, thabiti. Alikuwa halisi. Kijana wa pili hakuwa kama yule wa kwanza kabisa. Alikuwa mwenye kiburi na majivuno, na nilipokuwa ninazungumza naye ono lilipitia kwenye macho yangu nami nikaona ya kwamba alikuwa ameoa bibi mwenye nywele za shaba lakini alikuwa anaishi na mwingine mwenye nywele nyeusi na alikuwa amezaa

watoto wawili nae. Kama kulikuwako na mnafiki, alikuwa mmoja.

Sasa hebu niwaambie, nilishtuka sana. Vipi nisiweze kushtuka? Hapa palikuwa na watu wawili, mmoja wao ambaye alikuwa ni mwamini halisi na huyo mwingine alikuwa ni mwigaji mwenye dhambi. HATA HIVYO WOTE WAWILI WALIKUWA WAKIDHIHIRISHA KARAMA ZA ROHO. Nilisumbuliwa na mchafuko huu. Nikaondoka mkutanoni nipate kumtafuta Mungu anipe jibu. Nikaenda peke yangu mahali pa siri na hapo nikiwa na Biblia yangu nikaomba na kumngojea Mungu anipe jibu. Nikiwa sijui tu nisome sehemu gani ya Maandiko nilijifungulia tu Biblia mahali fulani katika Mathayo. Nilisoma kwa kitambo kidogo kisha nikaiweka Biblia chini. Haijapita muda kidogo upepo ukavuma kuingia mlechumbani na kuzigeuza kurasa za Biblia kwenye Waebrania, sura ya sita. Niliisoma yote na nikavutiwa sana na aya hizo za ajabu,

Waebrania 6:4-9,

*"Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu,*

*Na kulionja Neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo,*

*Wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamsulibisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri.*

*Maana nchi inayoinywa mvua inayoinyeshea mara kwa mara, na kuzaa mboga zenye manufaa kwa hao ambao kwa ajili yao yalimwa, hushiriki baraka zitokazo kwa Mungu;*

*Bali ikitoa miiba na magugu hukataliwa na kuwa karibu na laana; ambayo mwisho wake ni kuteketezwa.*

*Lakini, wapenzi, ijapokuwa twanena hayo, katika habari zenu tumesadiki mambo yaliyo mazuri zaidi, na yaliyo na wokovu."*

Niliifunga Biblia, nikaiweka chini, na kutafakari kwa muda kidogo na kuomba zaidi. Bado sikuwa na jibu. Nikaifungua Biblia tena bila kufikiria lakini sikuisoma. Mara upepo ukavuma kuingia mle chumbani tena, na mara nyingine tena kurasa zikafunguka kwenye Ebr. sita na kubakia hapo wakati upepo ulipokoma. Nilisoma maneno hayo tena, na nilipoyasoma, ndipo Roho wa Mungu akaingia chumbani na nikaona ono. Nikaona katika ono mtu aliyevaa nguo nyeupe sana ambaye alitoka akaenda kwenye shamba lililolimwa karibuni na kupanda mbegu. Ilikuwa ni siku isiyo na mawingu, na upanzi ulifanyika asubuhi. Lakini usiku ulipokuwa umeenda sana baada ya yule mpanzi aliyevalia mavazi meupe kuondoka, mtu aliyevaa mavazi meusi akaja akapanda kifichifichi mbegu nyingine kati ya zile yule mtu aliyevaa mavazi meupe alikuwa amepanda. Siku zikapita_jua na mvua vikaibariki nchi; na siku moja ile nafaka ikatokeza. Jinsi ilivyokuwa nzuri. Lakini siku moja baadaye yakaonekana magugu.

Ngano na magugu vikakua pamoja. Vikashiriki chakula kile kile kutoka katika ardhi ile ile. Vikanywa kutoka kwenye jua lile lile na mvua.

Ndipo siku moja mbingu zikageuka kuwa shaba, na mimea yote ikaanza kuanguka na kufa. Nikasikia ngano ikiinua vichwa vyao na kumlilia Mungu ipate mvua. Magugu pia yaliinua sauti zao na kusihi yapate mvua. Ndipo mbingu zikawa nyeusi na mvua ikaja, na mara nyingine tena ile ngano, ikiwa sasa imejaa nguvu ikainua sauti yake katika sifa, "Bwana asifiwe." Na kwa mshangao wangu nikasikia magugu yaliyokuwa yamehuishwa pia yakiangalia juu na kusema, "Haleluya!"

Ndipo nikajua ukweli wa ule mkutano wa kambi na lile ono. Ule mfano wa Mpanzi pamoja na Mbegu, sura ya sita ya Waebrania, na dhihirisho dhahiri la karama za Kiroho katika kusanyiko lililochanganyikana_yote yakawa dhahiri vizuri sana. Mpanzi aliyevaa nguo nyeupe alikuwa ni Bwana. Mpanzi aliyevaa nguo nyeusi alikuwa ni ibilisi. Ulimwengu ulikuwa shamba. Mbegu hizo zilikuwa ni watu, wateule na waliokataliwa. Wote wawili walikula chakula kile kile, maji na jua. Wote wawili waliomba. Wote walipata msaada kutoka kwa Mungu, kwa kuwa huwaangazia jua Lake na kunyeshea mvua Yake wenye haki na wasio haki. Na ingawa wote walikuwa na baraka zile zile za ajabu, na wote wawili walikuwa na madhihirisho mazuri sana, KULIKUWA KUNGALI NA ILE TOFAUTI MOJA, WALIKUWA NI WA MBEGU TOFAUTI.

Hapa pia kulikuwa na jibu la Mathayo 7:21-23

*"Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba Yangu Aliye mbinguni.*

*Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa Jina Lako, na kwa Jina Lako kutoa pepo, na kwa Jina Lako kufanya miujiza mingi?*

*Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni Kwangu, ninyi mtendao*

*maovu."*

Yesu hakatai kwamba walifanya kazi kuu ambazo ni Roho Mtakatifu pekee anayeweza kutimiza kwa njia ya wanadamu. Lakini Yeye alikataa kuwajua kamwe. Hawa hawakuwa wamerudi nyuma. Hawa walikuwa watu waovu, wasioongoka, waliokataliwa. Hawa walikuwa ni uzao wa Shetani.

Na ndio hilo hapo. HUWEZI kudai ya kwamba dhihirisho ndio ushuhuda wa kuzaliwa na Roho, kujazwa na Roho. Hapana bwana. Nitakubali ya kwamba dhihirisho la kweli ni ushuhuda wa Roho Mtakatifu akifanya kazi kuu, lakini SI thibitisho la yule mtu binafsi kujazwa na Roho, hata ingawa mtu huyo binafsi ana wingi wa madhihirisho hayo.

Ushuhuda wa kumpokea Roho Mtakatifu leo ni kama vile vile tu ilivyokuwa kule nyuma katika siku za Bwana wetu. Ni kupokea Neno la kweli kwa ajili ya siku unayoishi. Yesu kamwe hakutilia mkazo umuhimu wa Kazi kama alivyotilia maanani sana Neno. Alijua ya kwamba kama watu wakipata NENO kazi hizo zingefuata. Hiyo ni Biblia.

Sasa Yesu alijua ya kwamba kutakuweko na kutoka kwenye Neno kubaya sana katika Wakati wa Pergamo ambao ulikuwa bado umbali wa miaka mia mbili kutoka kwenye lile ono la Patmo. Alijua ya kwamba kutoka huko kungewafanya kuingia katika zile Zama za Giza. Yeye alijua ya kwamba jinsi mwanadamu alivyomwacha Mungu hapo mwanzo ilikuwa kwa kuliacha Neno kwanza. Kama ukiacha hilo Neno, umemwacha Mungu. Kwa hivyo Yeye anajionyesha mwenyewe kwa kanisa la Pergamo, na kwa kweli kwa makanisa yote ya nyakati zote, "Mimi ni Neno. Kama unataka Uungu katikati yako, basi likaribishe na ulipokee Neno. Kamwe usimwache mtu ye yote ama cho chote kiingie kati yako na hilo Neno. Hili ninalowapa (Neno) ni ufunuo wa Mimi Mwenyewe. MIMI NI NENO. Kumbukeni jambo hilo!"

Sijui kama tumeguswa moyoni na Neno vya kutosha lililoko katikati yetu. Hebu niwape wazo hapa. Tunaombaje? Tunaomba katika Jina la Yesu, sivyo? Kila maombi yamo katika Jina Lake ama hakuna jibu lo lote.

Hata hivyo katika I Yohana 5:14, tunaambiwa,

> *"Na huu ndio ujasiri tulio nao Kwake, ya kuwa, tukiomba kitu cho chote sawasawa na mapenzi Yake, Yeye atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba."*

Sasa tunauliza, "Mapenzi ya Mungu ni nini?" Kuna njia moja tu ya kujua mapenzi Yake na hiyo ni kwa NENO LA MUNGU.

Maombolezo 3:37,

> *"Ni nani asemaye Neno nalo likafanyika, ikiwa Bwana hakuliagiza?"*

Hilo hapo. Kama haliko kwenye Neno huwezi kulipata. Kwa hiyo hatuwezi kuomba isipokuwa jambo liwe liko katika Neno, wala hatuwezi kusihi ama kuomba isipokuwa iwe ni katika Jina Lake. Hilo hapo tena. YESU (lile Jina) ni NENO (mapenzi). Huwezi kumtenganisha Mungu na Neno. Wao ni MMOJA.

Sasa basi, hili Neno alililoliacha nyuma kwenye ukurasa uliopigwa chapa ni sehemu Yake unapolikubali kwa imani katika maisha yaliyojazwa Roho. Yeye alisema ya kwamba Neno Lake lilikuwa ni uzima. Yohana 6:63b. Lakini hivyo ndivyo alivyo hasa:

Yohana 14:6,

> *"Mimi Ndimi Njia, Kweli na Uzima."*

Warumi 8:9b

> *"Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si Wake."*

Hilo hapo, Yeye ni Roho na Yeye ni Uzima. Hivyo ndivyo Neno lilivyo hasa; hivyo ndivyo Yesu alivyo hasa. Yeye ni Neno. Kwa hiyo wakati mtu aliyezaliwa na Roho, mtu aliyejazwa na Roho katika imani anapoingiza Neno hilo moyoni mwake na kuliweka midomoni mwake, mbona hilo ni sawa na Uungu ukinena. Kila mlima hauna budi kuondoka. Shetani hawezi kusimama mbele ya mtu huyo.

Kama kanisa, huko nyuma kabisa katika ule wakati wa tatu lilikuwa tu limeshikilia ule ufunuo wa Neno lililo hai katikati yao, nguvu za Mungu hazingefifia kama zilivyofifia katika zile Zama za Giza. Na leo hii, wakati kanisa linaporudi kwenye Neno katika imani, tunaweza kusema bila tashwishi ya kwamba utukufu wa Mungu na matendo ya ajabu ya Mungu yatakuwa katikati yake tena.

Usiku mmoja nilipokuwa nikimtafuta Bwana, Roho Mtakatifu aliniambia nichukue kalamu yangu niandike. Nilipoishika kalamu kuandika, Roho Wake alinipa ujumbe kwa ajili ya kanisa. Ninataka kuwaletea … Unahusu na Neno na bibi-arusi.

*"Haya hapa yale ninayojaribu kuwaambia. "Haya ndiyo ninayojaribu kuwaambieni. Sheria ya kuzaa ni kwamba kila jamii izae kwa jinsi yake yenyewe, yaani kulingana na Mwanzo 1:11, "Mungu akasema, Nchi na itoe majani, mche utoao mbegu, na mti wa matunda uzaao matunda kwa jinsi yake, ambao mbegu zake zimo ndani yake, juu ya nchi: ikawa hivyo." Uhai wo wote ule uliokuwemo katika mbegu ulijitokeza katika mmea na baadaye katika tunda. Sheria iyo hiyo inatenda kazi kwa kanisa leo. Mbegu yo yote iliyoanzisha kanisa itamea na kuwa kama ile mbegu ya asili kwa sababu ni mbegu ile ile. Katika siku hizi za mwisho Kanisa la Bibi-arusi wa kweli (mzao wa Kristo) litafikia kwenye Jiwe la Kileleni, nalo litakuwa ni kipeo cha kanisa, mzao bora sana, linapomkaribia Yeye. Wao katika Bibi-arusi watakuwa chapa Yake hivi kwamba watafanana Naye kabisa. Hii ni kusudi wapate kuungana Naye. Watakuwa mmoja. Watakuwa dhihirisho lenyewe la Neno la Mungu aliye hai. Madhehebu hayawezi kuleta hili (wao ni uzao mbaya). Wataleta kanuni zao za imani na mafundisho yao ya sharti, yaliyochanganywa na Neno. Mchanganyiko huu huzaa mzao mchanganyiko.*

*Yule mwana wa kwanza (Adamu) alikuwa ni mzao_Neno lililonenwa na Mungu. Alipewa bibi-arusi kusudi azaliane. Hiyo ndiyo sababu yeye alipewa bibi-arusi, apate kuzaliana, amzae mwana mwingine wa Mungu. Lakini huyo mwanamke alianguka. Alianguka kwa kuchanganya mbegu. Alisababisha mumewe afe.*

*Mwana wa pili (Yesu), pia Mzao-Neno lililonenwa na Mungu alipewa bibi-arusi kama vile Adamu alivyopewa. Lakini kabla hajaweza kumwoa, yeye pia alikuwa ameshaanguka. Yeye, kama vile mke wa Adamu, alijaribiwa kama angeliamini Neno la Mungu na aishi, au alitilie shaka Neno na afe. Alitilia shaka. Yeye aliliacha Neno. Alikufa.*

*Toka kwenye kundi dogo la mzao halisi wa Neno, Mungu atamtuza Kristo na bibi-arusi mzuri. Yeye ni bikira wa Neno Lake. Yeye ni bikira kwa sababu hazijui kanuni zo zote za imani zilizobuniwa na wanadamu wala mafundisho ya sharti. Kwa njia ya washirika na kupitia kwa washirika wa bibi-arusi yatatimizwa yale yote yaliyoahidiwa na Mungu kudhihirishwa katika bikira.*

*Neno la ahadi lilimjia bikira Mariamu. Lakini hilo Neno la ahadi lilikuwa ni Yeye, Mwenyewe, kudhihirishwa. Mungu alidhihirishwa. Yeye, Mwenyewe, alifanya tendo wakati huo na kulitimiza Neno Lake la ahadi katika huyo bikira. Malaika ndiye aliyemletea ujumbe. Lakini ujumbe wa malaika ulikuwa ni Neno la Mungu. Isaya 9:6. Yeye aliyatimiza wakati huo yote yale yaliyoandikiwa Yeye kwa sababu huyo bikira alilikubali Neno Lake alilomletea.*

*Washiriki wa bibi-arusi bikira watampenda Yeye, nao watakuwa na uweza Wake, kwa maana Yeye ndiye kichwa chao, na nguvu zote ni Zake. Wanamtii Yeye kama vile viungo vya miili yetu vinavyotii vichwa vyetu.*

*Angalia kupatana kwa Baba na Mwana. Yesu hakufanya lo lote mpaka alipoonyeshwa jambo hilo kwanza na Baba. Yohana 5:19. Kupatana huku kunatakiwa sasa kuwepo kati ya Bwana Arusi na bibi-arusi Wake. Yeye humwonyesha Neno Lake la uzima. Naye analipokea. Yeye kamwe hatilii shaka. Kwa hiyo, hakuna kitu kinachoweza kumdhuru, wala hata mauti. Kwa kuwa kama mbegu imepandwa, maji yataifufua tena. Siri ya jambo hili ndiyo hii: Neno liko ndani ya bibi-arusi (kama ilivyokuwa katika Mariamu). Bibi-arusi ana nia ya Kristo kwa kuwa anajua kile anachotaka kifanyike kwa Neno. Anatekeleza maagizo ya Neno katika jina Lake kwa kuwa yeye anayo "Bwana asema hivi." Ndipo Neno linahuishwa na Roho nalo linatimia. Kama vile mbegu ambayo imepandwa na kumwagiwa maji, inafikia mavuno kamili, ikitimiza kusudi lake.*

*Wale walio katika bibi-arusi hufanya mapenzi Yake tu. Hakuna mtu anayeweza kuwafanya wafanye vinginevyo. Wao wana 'hivi asema Bwana' ama wanatulia. Wanajua ya kwamba hapana budi iwe ni Mungu ndani yao anayefanya hizo kazi, akilitimiza Neno Lake Mwenyewe. Yeye hakumaliza kazi Zake zote alipokuwa katika huduma Yake ya duniani kwa hivyo sasa Yeye hutenda kazi katika na kwa kupitia kwa bibi-arusi.*

*Bibi-arusi ajua hayo, kwa sababu wakati Wake wa kufanya mambo fulani ambayo hana budi kuyafanya sasa haukuwa umewadia. Lakini sasa Yeye atatimiza kupitia kwa bibi-arusi kazi ile aliyoiacha ili ifanywe kwa wakati huu uliokusudiwa.*

*Sasa hebu na tusimame kama Yoshua na Kalebu. Nchi yetu ya ahadi imeanza kuonekana kama vile yao ilivyoanza kuonekana. Sasa Yoshua maana yake ni "Yehova-Mwokozi," naye anamwakilisha kiongozi wa wakati wa mwisho ambaye atakuja kwa kanisa kama vile Paulo alivyokuja kama kiongozi wa kwanza. Kalebu anawakilisha wale waliodumu waaminifu kwa Yoshua. Kumbuka, Mungu alikuwa amewaanzisha Israeli kama bikira kwa Neno Lake. Lakini wao walitaka kitu tofauti. Vivyo hivyo na kanisa la siku za mwisho. Angalia jinsi ambavyo Mungu hakuwasogeza Israeli, au kuwaacha waingie katika nchi ya ahadi mpaka wakati Wake Mwenyewe uliokusudiwa ulipowadia. Sasa huenda hao watu walimsonga Yoshua, aliyekuwa kiongozi, na kusema, "Hiyo nchi ni yetu, hebu na twende tukaitwae. Yoshua, umeshindwa, lazima umepoteza agizo lako, huna ile nguvu uliyokuwa nayo. Ulikuwa ukisikia kutoka kwa Mungu na kujua mapenzi ya Mungu, na kutenda kwa haraka. Una kasoro." Lakini Yoshua alikuwa nabii aliyetumwa*

*na Mungu naye alijua ahadi za Mungu, kwa hiyo alizingojea. Yeye alingojea uamuzi dhahiri toka kwa Mungu na wakati ulipofika wa kusonga mbele, Mungu aliuweka uongozi mzima katika mikono ya Yoshua kwa sababu alikuwa amedumu na Neno. Mungu angeweza kumwamini Yoshua lakini si hao wengine. Kwa hiyo itajirudia katika siku hizi za mwisho. Shida ile ile, mashinikizo yale yale.*

*Chukua mfano tunaouona katika Musa. Nabii huyu wa Mungu mwenye nguvu aliyetiwa mafuta alizaliwa kiajabu, akiwa amezaliwa kwa wakati uliofaa kwa ajili ya ukombozi wa mzao wa Ibrahimu toka Misri. Yeye hakukaa Misri hata kidogo kuhojiana nao kwa Maandiko, wala kuzozana na makuhani. Alienda nyikani mpaka watu walikuwa tayari kumpokea. Mungu alimwita Musa nyikani. Kungoja kule hakukuwa kwa Musa bali ni kwa sababu ya watu waliokuwa hawajawa tayari kumpokea. Musa alifikiri watu wangeelewa lakini hawakuelewa.*

*Halafu kuna Eliya ambaye Neno la Bwana lilimjia. Alipomaliza kuhubiri kweli na hilo kundi zamani zile ambalo ni mtangulizi wa kundi la Yezebeli wa Marekani halingelipokea Neno! Mungu alimwita aondoke kwenye huduma kisha akakipiga mapigo kizazi hicho kwa ajili ya kumkataa nabii na ujumbe ambao Mungu ameutangaza. Mungu alimwita aende nyikani naye hangetokea hata kama angeitwa na mfalme. Wale waliojaribu kumshawishi afanye hivyo, walikufa. Lakini Mungu alinena na nabii Wake mwaminifu kwa ono. Toka mafichoni alikuja na kuwarejeshea Neno Israeli.*

*Ndipo akaja Yohana Mbatizaji, mtangulizi mwaminifu wa Kristo, nabii mwenye nguvu kwa ajili ya siku yake. Hakwenda kwenye shule ya baba yake, wala kwenye shule ya Mafarisayo_hakwenda kwenye madhehebu yo yote, bali alienda huko nje nyikani alikoitwa na Mungu. Akakaa huko mpaka Mungu alipomtuma akiwa na ujumbe, akapaza sauti, „Masihi amekaribia."*

*Sasa hebu tuchukue onyo la Kimaandiko hapa. Je! haikuwa ni katika siku za Musa ambaye Mungu alikuwa amemthibitisha ambapo Kora aliinuka na kumpinga huyo nabii mkuu? Alibishana na Musa na kudai kuwa yeye pia alikuwa na mambo yale yale kutoka kwa Mungu kwa kuwaongoza hao watu na ya kwamba wengine walishiriki katika ufunuo wa Kiungu kama vile vile Musa alivyoshiriki. Alikana mamlaka ya Musa. Basi hao watu zamani zile, baada ya kulisikia Neno la kweli nao walifahamu vizuri kabisa ukweli kwamba nabii wa kweli alikuwa amethibitishwa na Mungu, nasema watu hao walimfuata Kora na ukaidi wake. Kora hakuwa nabii wa Kimaandiko bali umati mkubwa wa watu pamoja na viongozi wao walimfuata. Ni sawa vipi na wainjilisti siku hizi wakiwa na maazimio yao ya ndama wa dhahabu kama wa Kora. Wanaonekana wazuri kwa watu kama vile Kora alivyoonekana wakati huo. Wana damu katika paji za nyuso zao, mafuta mikononi mwao na mipira ya moto jukwaani. Wanaruhusu wahubiri wanawake, wanawaruhusu wanawake wanyoe nywele zao, wavae suruali na kaptura, na kulivuka Neno la Mungu kwa kutimiliza kanuni zao wenyewe za imani na mafundisho ya sharti. Hiyo inaonesha ni aina gani ya mbegu iliyo ndani yao. Bali sio watu wote waliomkataa Musa na kuliacha Neno la Mungu. La. Wateule walikaa pamoja naye. Jambo lile lile linatukia tena leo hii. Wengi wanaacha Neno lakini wengine wanakaa nalo. Lakini kumbuka mfano wa ngano na magugu. Magugu hayana budi kukusanywa matita matita yakachomwe moto. Makanisa haya yenye kukana imani yanafungwa pamoja na kukazwa zaidi na zaidi, tayari kwa ajili ya mioto ya hukumu ya Mungu. Lakini ngano itakusanywa kwa Bwana.*

*Sasa ninawatakeni muwe waangalifu sana hapa na mwone jambo hili. Mungu ameahidi ya kwamba katika wakati wa mwisho Malaki 4 itatimizwa. Haina budi kutimia kwa kuwa ni Neno la Mungu lililohuishwa na Roho lililonenwa na nabii Malaki. Yesu alilitaja hilo. Ni kabla tu ya Kristo kuja mara ya pili. Ifikapo wakati wa kuja Kwake Yesu Maandiko yote hayana budi kutimizwa. Kipindi cha Mataifa kitakuwa kimefikia wakati wake wa kanisa la mwisho wakati huyo mjumbe wa Malaki atakapokuja. Yeye atakuwa amesimama na Neno kweli kweli. Yeye ataichukua Biblia nzima kutoka Mwanzo hadi Ufunuo. Ataanzia kwenye uzao wa nyoka na kuendelea hata kwenye mjumbe wa mvua ya masika. Lakini yeye atakataliwa na madhehebu.*

*Yeye hana budi kuwa kwa kuwa hiyo ni historia inayojirudia yenyewe tangu wakati wa Ahabu. Historia ya Israeli chini ya uongozi wa Ahabu inatimia papa hapa Marekani ambapo nabii wa Malaki anatokea. Kama vile Israeli walivyoondoka Misri waende wakaabudu kwa uhuru, wakawafukuza wenyeji, wakaunda taifa lenye viongozi mashujaa kama Daudi nk., kisha wakamweka Ahabu kwenye kiti cha enzi na Yezebeli nyuma yake akimwongoza, vivyo hivyo tumefanya jambo lile lile Marekani. Babu zetu walikuja katika nchi hii wapate kuabudu na kuishi katika uhuru. Waliwafukuza wenyeji na kuitwaa nchi. Watu wenye nguvu kama vile Washington na Lincoln waliinuliwa lakini baadaye kidogo watu wengine wasiofaa waliwafuatia watu hawa mashuhuri hata punde si punde Ahabu aliwekwa kwenye kiti cha urais na Yezebeli nyuma yake kumwongoza. Ni katika wakati kama huu ambapo mjumbe wa Malaki hana budi kuja. Ndipo katika mvua ya vuli kutatokea shindano dhahiri la Mlima Karmeli. Angalia jambo hili kwa makini sasa kuliona katika Neno. Yohana alikuwa mtangulizi wa Malaki 3. Yeye alipanda mvua ya masika na kukataliwa na mashirika ya siku zake. Yesu alikuja na akawa na shindano la Mlima wa Kugeuka Sura. Mtangulizi wa pili wa Kristo atapanda kwa ajili ya mvua ya vuli. Yesu atakuwa shindano kati ya madhehebu na kanuni za imani, kwa kuwa Yeye atakuja kuliunga mkono Neno Lake na kumtwaa bibi-arusi Wake katika unyakuo. Shindano la kwanza lilikuwa kwenye Mlima Karmeli; la pili lilikuwa kwenye Mlima wa Kugeuka Sura, na la tatu litakuwa kwenye Mlima Sayuni.*

*Tabia ya ajabu ya Musa, Eliya, na Yohana ya kujitenga na watu na kuishi katika upweke iliwaacha wengi wametatanika. Wao hawakutambua kwamba ni kwa sababu jumbe zao zilikuwa zimekataliwa. Lakini mbegu ilikuwa imepandwa, kupanda kulikuwa kumemalizika. Hukumu ilikuwa inafuata. Walikuwa wamemaliza kazi yao kama ishara kwa watu, kwa hiyo hukumu ilikuwa inafuata.*

*Ninaamini kulingana na Ufu. 13:16 ya kwamba itambidi bibi-arusi kuacha kuhubiri kwa maana yule mnyama anadai chapa katika mkono au paji la uso ikiwa ruhusa ya kuhubiri itatolewa. Madhehebu yataichukua ile chapa, la sivyo yatalazimishwa kuacha kuhubiri. Ndipo Mwana-Kondoo atakuja kumchukua bibi-arusi Wake na kumhukumu yule kahaba mkuu.*

*Sasa kumbuka ya kwamba Musa alizaliwa kwa ajili ya kazi fulani, lakini asingeweza kufanya kazi hiyo mpaka awe amepokea karama ambazo zingemwezesha kufanya kazi hiyo. Ilimbidi kwenda jangwani na kungojea kule; Mungu alikuwa na wakati aliouchagua. Kulikuwa kuwe na Farao fulani kwenye kiti cha enzi, na iliwapasa watu wawe wakililia mkate wa uzima, kabla ya Mungu hajamrudisha. Ni vivyo hivyo katika siku zetu.*

*Lakini tuna nini katika siku hii yetu? Umati mkubwa unafanya ishara mpaka tuna kizazi cha watafuta ishara wanaojua machache ama wasiojua lo lote kuhusu Neno, au tendo halisi la Roho wa Mungu. Wao wakiona damu, mafuta na moto wanasikia kubarikiwa; haidhuru ni kitu gani kilichoko katika Neno. Wao wataunga mkono ishara yoyote, hata isiyo ya kimaandiko. Lakini Mungu ametuonya juu ya jambo hilo. Yeye alisema katika Mathayo 24 kwamba katika siku za mwisho zile roho mbili zitafanana sana hivi kwamba ni walio wateule tu wangeweza kuzitofautisha, kwa kuwa hao pekee ndio ambao hawatadanganywa.*

*Unaweza kuzitofautisha roho hizo? Hebu zipe tu jaribio la Neno. Kama hazizungumzi hilo Neno, ni za yule mwovu. Kama vile yule mwovu alivyowadanganya wale bibi-arusi wawili wa kwanza, yeye atajaribu kumdanganya bibi-arusi wa siku hii ya mwisho, kwa kujaribu kumfanya ajichanganye mbegu katika kanuni za imani, ama tu kuliacha Neno wazi wazi na kufuata ishara yo yote inayomfaa. Lakini Mungu kamwe hakuweka ishara mbele ya Neno. Ishara hufuata Neno, kama wakati ule wa Eliya alipomwambia yule mwanamke amtengenezee mkate kwanza, kulingana na Neno la Bwana. Wakati alipofanya kama Neno lilivyosema, ishara halisi ilikuja. Njoo kwenye Neno kwanza kisha uone muujiza. Mbegu Neno hutiwa nguvu na Roho.*

*Yawezekanaje mjumbe ye yote aliyetumwa toka kwa Mungu kuamini tu sehemu ya Neno na kukana sehemu nyingine? Nabii wa kweli wa Mungu katika siku hii ya mwisho atalitangaza Neno lote. Madhehebu yatamchukia. Maneno Yake huenda yakawa makali kama Yohana Mbatizaji aliyewaita nyoka. Lakini wale waliochaguliwa tangu zamani watasikia na kuwa tayari kwa ajili ya kunyakuliwa. Mzao wa Kifalme wa Ibrahimu, ukiwa na imani kama ya Ibrahimu watalishikilia hilo Neno pamoja naye, kwa kuwa wao walichaguliwa tangu awali pamoja naye.*

*Mjumbe wa siku ya mwisho atatokea katika wakati uliokusudiwa na Mungu. Ni wakati wa mwisho sasa kama wote wanavyojua, kwa maana Israeli wako katika nchi yao. Wakati wowote sasa atakuja kulingana na Malaki. Tutakapomwona, atakuwa amefungwa kwenye Neno. Naye atadhihirishwa (ataonyeshwa wazi katika Neno. Ufunuo 10:7.) Na Mungu atathibitisha huduma yake. Atahubiri ukweli kama vile Eliya alivyofanya na kuwa tayari kwa shindano la Mlima Sayuni.*

*Wengi hawatamfahamu kwa sababu wamefundishwa Maandiko kwa njia fulani ambayo wao hufikiria ndiyo kweli. Wakati ajapo kinyume cha hilo, hawataamini. Hata wahudumu wengine wa kweli watakosa kumwelewa huyo mjumbe kwa sababu mengi sana yameitwa ukweli wa Mungu na watu wadanganyifu.*

*Lakini huyu nabii atakuja, na kama vile yule mtangulizi wa kule kuja kwa kwanza alivyopaza sauti, "Tazama Mwana- Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu, vivyo hivyo bila shaka naye atapaza sauti, "Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu anayekuja katika utukufu." Atafanya jambo hili, kwa maana kama vile Yohana alivyokuwa mjumbe wa ile kweli kwa wateule, ndivyo alivyo na huyu mjumbe wa mwisho kwa wateule na kwa bibi-arusi aliyezaliwa kwa Neno.*

**KRISTO ALISIFU KANISA**

Ufunuo 2:13

> *"Nayajua matendo yako, na napajua ukaapo, ndipo penye kiti cha enzi cha Shetani; nawe walishika sana Jina Langu, wala hukuikana imani yangu, hata katika siku za Antipa shahidi Wangu, mwaminifu Wangu, aliyeuawa katikati yenu, hapo akaapo Shetani.*

*"Nayajua matendo yako."* Haya ni maneno yanayofanana anayoambiwa kila mmoja wa wale wajumbe saba kuhusiana na watu wa Mungu katika kila wakati. Yanaponenwa kwa ile mizabibu miwili (wa kweli na wa uongo) yataleta furaha na shangwe kwa mioyo ya kundi moja, lakini yanapaswa kutia kishindo cha hofu kuu katika mioyo ya hilo jingine. Kwa maana ingawa tunaokolewa kwa neema, mbali na matendo, wokovu wa kweli utazaa matendo, ama matendo ambayo yatamfurahisha Mungu.

I Yohana 3:7,

*"Watoto wadogo, mtu na asiwadanganye; ATENDAYE (afanyaye) haki yuna haki, kama Yeye alivyo na haki."*

Kama aya hii ina maana yo yote hata kidogo, inamaanisha ya kwamba kile mtu AFANYACHO ndicho ALICHO.

Yakobo 3:11,

*"Je! chemchemi katika jicho moja hutoa maji matamu na maji machungu?"*

Warumi 6:2,

*Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?*"

Mathayo 12:33-35

*"Ufanyeni mti kuwa mzuri na matunda yake kuwa mazuri; au ufanyeni mti kuwa mbaya na matunda yake mabaya, kwa maana kwa matunda yake mti hutambulikana.*

*Enyi wazao wa nyoka, mwawezaje kunena mema, mkiwa wabaya? Maana, kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake.*

*Mtu mwema katika akiba njema ya moyo hutoa mema; na mtu mbaya katika akiba mbaya hutoa mabaya.*"

Sasa kama mtu amezaliwa kwa Neno (Mkizaliwa mara ya pili, si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika; kwa Neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele. I Pet. 1:23) yeye atadhihirisha Neno. Matunda ama matendo ya maisha yake yatakuwa ndiyo matokeo ya namna ya mbegu ama uhai ulio ndani yake. Hivyo basi matendo yake yatakuwa ya Kimaandiko. Loo! kweli hii itakuwa ni shtaka la namna gani dhidi ya Wakati wa Pergamo. Huyo hapo anasimama Yeye Asiye na Kifani, na katika mkono Wake kuna upanga mkali wenye makali kuwili, Neno la Mungu. Na Neno hilo litatuhukumu katika siku ya mwisho. Kwa kweli Neno linahukumu hata sasa hivi, kwa maana huyatambua mawazo na makusudi ya moyo. Linakata na kuwatenga wa kimwili na wa kiroho. Linatufanya nyaraka zilizo hai na zinazojulikana na watu wote kwa utukufu wa Mungu.

*"Nayajua matendo yako."* Kama mtu akihofu kwamba huenda asimpendeze Mungu, basi na alitimize Neno. Kama mtu hajui kama atayasikia maneno hayo, "Vema, mtumwa mwema na mwaminifu," hebu na alitimize Neno la Mungu katika maisha yake, na bila shaka atayasikia maneno hayo ya sifa. Neno la kweli ndilo lililokuwa kigezo wakati huo; ndicho kigezo sasa. Hakuna kipimo kingine; hakuna timazi nyingine. Kwa kuwa ulimwengu utahukumiwa na Kristo Yesu, vivyo hivyo utahukumiwa kwa Neno. Kama mtu akitaka kujua jinsi anavyofanikiwa, hebu na afanye kama Yakobo alivyoshauri: "Angalia katika kioo cha Neno la Mungu."

*"Nayajua matendo yako."* Alipokuwa amesimama pale na Neno Lake, akiyachunguza maisha yao katika nuru ya kielelezo alichokuwa amewapa, hana budi alifurahishwa kiasi, kwa sababu wao, kama wale wengine waliowatangulia, walikuwa wanayastahimili mateso ya wasio haki na huku wangali kwa furaha wanamshikilia Bwana. Ingawa wakati mwingine ilikuwa ni vigumu kumtumikia Bwana, hata hivyo wao walimtumikia na kumwabudu Yeye katika Roho na katika kweli. Lakini kwa mzabibu wa uongo haikuwa hivyo. Loo! walikuwa wameyakataa maisha yanayojengwa juu ya Neno na sasa wao walikuwa wanaendelea kuiacha kweli. Matendo yao yalishuhudia kilindi walichokuwa wamezama.

## WEWE WALISHIKA SANA JINA LANGU

*"Twende kwa nani? Wewe peke yako unayo maneno ya uzima wa milele!"* Walishikilia sana wakati huo; walikuwa wakishikilia sana sasa, lakini si kwa hofu ya kukata tamaa kama watu wanaoishi maisha ya bure. Walikuwa wakishikilia sana katika nguvu Zake, katika uhakikisho wa Roho ya kwamba wao walikuwa mmoja katika Yeye. La kwao lilikuwa ni ufahamu wa hakika wa dhambi zilizosamehewa nao walikuwa na jina la „Mkristo" katika kulishuhudia jina hilo. Walilijua na kulipenda Jina lile ambalo lilipita kila jina. Magoti yao yalipigwa kwa Jina Hilo. Ndimi zao zilikwishalikiri. Lo lote walilotenda, walitenda yote katika Jina la Bwana Yesu. Walikuwa wameliitia Jina hilo na wakaacha uovu, na baada ya kuchukua msimamo wao walikuwa sasa wako tayari kufa kwa ajili ya Jina hilo, wakiwa wamehakikishiwa ufufuo bora.

Peleka Jina la Yesu,
Mtoto wa huzuni na shida.
Litakuwa furaha na faraja.
Lipeleke kila mahali uendako.
Jina la thamani, Lo ni tamu iliyoje,
Tumaini la duniani na furaha ya mbinguni.

Tayari katika karne ya pili maneno hayo "Baba, Mwana na Roho Mtakatifu" yalikuwa yameandika neno „Utatu" kwa wengi, na wazo la imani ya miungu mingi la Miungu watatu lilikuwa tayari limekuwa ni fundisho katika kanisa la uongo. Haikuchukua muda mrefu hata lile Jina lilipokuwa limeondolewa, kama kweli lilivyoondolewa katika wakati huu, na mahali pake zile sifa za yule MUNGU MMOJA MKUU zingewekwa badala ya lile JINA, Bwana Yesu Kristo. Wakati wengi walikana imani na kushika utatu na kubatiza wakitumia zile sifa za Mungu, lile Kundi Dogo bado lilibatiza katika Jina la Yesu Kristo na hivyo lilishikilia kweli.

Huku wengi sana wakimdharau Mungu, wakimbadilisha kuwa miungu watatu, na kulibadilisha Jina Lake la neema na kulifanya sifa, mtu angeshangaa kama ishara na maajabu yanayoambatana na Jina kubwa kama hili yangeonekana kati ya watu. Kweli ishara hizo zilidhihirishwa kwa nguvu na kwa ajabu sana, ingawa bila shaka si katika ule mzabibu wa uongo. Watu kama Martin walitumiwa sana na Mungu aliwashuhudia kwa ishara na maajabu pia na karama za Roho Mtakatifu. Jina hilo bado lilikuwa linatenda kazi kama vile lilivyokuwa daima na litakavyokuwa daima ambapo watakatifu wanamheshimu Yeye kwa Neno na imani.

**WEWE HUKUIKANA IMANI YANGU**

Katika Mdo. 3:16 wakati Petro alipoulizwa jinsi ule mwujiza mkuu ulivyokuwa umetukia kwa yule kiwete kwenye ule Mlango Mzuri, yeye aliuelezea namna hii, *"Na kwa imani katika Jina Lake (Yesu), Jina Lake (Yesu) limemtia nguvu mtu huyu (aliyekuwa kiwete) mnayemwona na kumjua; naam imani ile iliyo (inayotoka) Kwake Yeye (Yesu) imempatia huyu (yule mtu) uzima huu mkamilifu mbele yenu ninyi nyote."* Mnaona, ndivyo ilivyo. *Jina la Yesu, na Imani ya Yesu ilisababisha huo muujiza. Petro hakudai ilikuwa ni imani yake ya kibinadamu zaidi ya kudai ya kwamba ilikuwa ni jina lake mwenyewe. Alisema ya kwamba Jina la Yesu likitumiwa katika imani inayotoka kwa Yesu ndiyo iliyotenda kazi hiyo kuu. Imani hii ndiyo Bwana aliyokuwa akinena habari zake katika Ufu. 2:13. Ilikuwa ni imani YAKE. Haikuwa imani KATIKA Yeye. Lakini ilikuwa ni imani YAKE MWENYEWE ambayo alikuwa amewapa waamini.*

Warumi 12:3

> *"Kama Mungu alivyomgawia kila mtu (kulingana na aya ya kwanza watu hapa ni NDUGU) kiasi cha imani."*

Waefeso 2:8,

> *"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo (Imani) haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu."*

Na pia inasema katika Yakobo 2:1,

> *"Ndugu zangu (angalia yeye, pia, anazungumza na NDUGU), imani YA (si katika) Bwana wetu Yesu Kristo, Bwana wa utukufu, msiwe nayo kwa kupendelea watu."*

Katika Wakati huu wa Pergamo ambapo watu walikuwa wakiufanya wokovu kuwa ni wa kibinadamu, baada ya kugeuka kutoka kwenye kweli kwamba "Wokovu ni wa Bwana,"_baada ya kutupilia mbali fundisho la kuteuliwa na kufungua wazi mlango wa kanisa na ushirika wao kwa ye yote na wote ambao wangekubaliana na mafundisho yao (bila kulijali Neno), katika wakati huu wa kuja upesi kwa ufisadi, kungali kulikuweko na wale wachache waliokuwa na kiasi cha ile imani ya Bwana wetu Yesu Kristo, na hawakutumia tu imani hiyo katika matendo ya nguvu lakini walishindana na hao waliothubutu kusema ya kwamba wameokoka ati kwa sababu tu walijiunga na kanisa. Walijua ya kwamba hakuna mtu ambaye kweli angaliamini apate uzima wa milele na haki ya Mungu mbali na kiasi cha imani ya Bwana Yesu, Mwenyewe. Kwa kuwa kanisa la leo limejaa waamini wa kiakili wanaokubaliana na kuzaliwa kibikira, ile damu iliyomwagwa, kuhudhuria kanisa na kushiriki meza ya Bwana, na hawajazaliwa mara ya pili hata kidogo, hata hivyo katika wakati ule wa tatu shida ilikuwa ni ile ile. Imani ya kibinadamu haikutosha wakati huo wala haitoshi sasa. Inahitaji imani yenyewe ya Mwana wa Mungu kushuka katika moyo wa mwanadamu ili kwamba aweze kumpokea Bwana wa utukufu katika hekalu lisilofanywa kwa mikono.

Hii ilikuwa ni imani iliyo hai. "Ninaishi kwa imani ya Mwana wa Mungu." Paulo hakusema aliishi kwa imani KATIKA Mwana wa Mungu. Imani ya Mwana wa Mungu ndiyo iliyokuwa imempa uzima na kumdumisha kuishi katika ushindi wa Kikristo.

La, wao hawakuwa wamekana ya kwamba wokovu ulikuwa wa rohoni tangu mwanzo hata mwisho. Waliichochea kweli ya Jina Lake na Imani Yake nao wakabarikiwa na Bwana na kuhesabiwa kwamba wanamstahili Yeye.

**ANTIPA SHAHIDI WANGU MWAMINIFU**

Hakuna kumbukumbu nyingine katika Neno au katika historia yo yote ya kilimwengu kumhusu ndugu huyu. Lakini hakika hakuna haja. Imetosha hata na zaidi ya wamba alijulikana tangu zamani na kujulikana

na Bwana. Imetosha hata na zaodo kuona uaminifu wake kwa Bwana umeandikwa katika Neno lililo hai. Yeye alikuwa ni Mkristo. Alikuwa na Jina la Yesu. Alikuwa na imani ya Bwana wetu Yesu Kristo na alikuwa miongoni mwa wale walioishi kwayo. Alikuwa ameitikia maneno ya Yakobo, "Imani ya Bwana wetu Yesu Kristo msiwe nayo kwa kupendelea watu." Akiwa amejaa Roho Mtakatifu na imani kama alivyokuwa Stefano, hakumpendelea mtu ye yote, hakumwogopa mtu; na hapo kifo kilipotangazwa juu ya wote ambao wangelichukua hilo Jina na kutembea katika imani ya Yesu Kristo yeye alichukua msimamo wake pamoja na wale ambao hawangegeuka nyuma. Naam, alikufa, lakini kama vile Habili, alipata ushuhuda kutoka kwa Mungu (jina lake limeandikwa katika Neno), na ingawa amekufa, sauti yake ingali inanena katika kurasa za Mungu za Kumbukumbu ya Mungu. Shahidi mwingine mwaminifu alipelekwa kwenye raha yake. Lakini Shetani hakushinda wakati huo, kama vile ambavyo hakushinda wakati alipomwua Mfalme wa Amani, kwa maana kama vile Shetani alivyonyang"anywa mamlaka msalabani, vivyo hivyo sasa damu ya Antipa itawalilia mamia zaidi watakaochukua misalaba yao na kumfuata Yeye.

**PENYE KITI CHA ENZI CHA SHETANI**

Sababu ya hii kuwa ni sehemu ya sifa za Roho ni kwamba hawa askari hodari wa msalaba walikuwa wanamshinda Shetani papo hapo katikati ya chumba chake mwenyewe cha kiti cha enzi. Walikuwa wanashinda vita kwa Jina na Imani ya Yesu katikati ya kambi ya viongozi wa giza. Ni sifa nzuri namna gani. Kama vile wale watu mashujaa wa Daudi ambao walivamia kambi ya adui kumletea Daudi maji yanayozima kiu, vivyo hivyo mashujaa hawa wa imani walivamia milki ya ngome ya duniani ya Shetani, na kwa kuhubiri na kuonya wakawaletea maji ya wokovu wale walioishi chini ya kivuli cha mauti.

Sasa kadiri maneno haya kuhusu kiti cha enzi na milki ya Shetani ni sehemu ya sifa za Mungu kwa wateule Wake, kwa kweli yaliweka jukwaa la mashambulizi juu ya uovu ambao ulitawala kanisani.

**PERGAMO:** *Kiti cha enzi cha Shetani na Makao Yake.* Kwa watu wengi, matamshi haya yamekuwa yanaonyesha picha tu wala si ya kihistoria kweli. Lakini hakika ni halisi na historia inashuhudia jambo hilo. Pergamo kweli ulikuwa ni kiti cha enzi na makao ya Shetani. Jambo hilo lilitukia hivi:

Pergamo hapo mwanzo haukuwa mahali ambapo Shetani (kuhusu mambo ya kibinadamu) alikaa. Babeli ndio daima umekuwa makao yake makuu halisi na kwa mfano wa makao yake makuu. Ibada za Kishetani zilianzia katika jiji la Babeli Mwa. 10:8-10, *"Kushi akamzaa Nimrodi, akaanza kuwa mtu hodari katika nchi. Alikuwa hodari kuwinda wanyama mbele za Bwana. Mwanzo wa ufalme wake ulikuwa Babeli na Ereku, na Akadi, na Kalne, katika nchi ya Shinari."*

Mwanzo 11:1-9,

> *"Nchi yote ilikuwa na lugha moja na usemi mmoja.*
>
> *Ikawa watu waliposafiri pande za mashariki kwamba waliona nchi tambarare katika nchi ya Shinari; na wakakaa huko.*
>
> *Wakaambiana, Haya, na tufanye matofali tukayochomea moto. Walikuwa na matofali badala ya mawe, na lami badala ya chokaa.*
>
> *Wakasema, Haya, na tujijengee mji, na mnara, na kilele chake kifike mbinguni, tujifanyie jina; ili tusipate kutawanyika usoni pa nchi yote.*
>
> *Bwana akashuka ili auone mji na mnara waliokuwa wakiujenga wanadamu.*
>
> *Ndipo Bwana akasema, Tazama, watu hawa ni taifa moja, na lugha yao ni moja; na haya ndiyo wanayoanza kuyafanya, wala sasa hawatazuiliwa neno wanalokusudia kulifanya.*
>
> *Haya, na tushuke huko, tuwachafulie usemi wao ili wasisikilizane maneno wao kwa wao.*
>
> *Basi Bwana akawatawanya kutoka huko waende usoni pa nchi yote; wakaacha kuujenga ule mji.*
>
> *Kwa sababu hiyo jina lake likaitwa Babeli; maana hapo ndipo Bwana alipoichafua lugha ya dunia yote; na kutoka huko Bwana akawatawanya waende usoni pa nchi yote."*

Bebeli ndilo jina la asili la Babeli. Linamaanisha mchafuko. Ulianzishwa hasa na Kushi, mwana wa Hamu, lakini ulifanywa ufalme wenye nguvu na fahari chini ya mwanawe, Nimrodi, yule mwindaji hodari. Nimrodi, kulingana na maelezo ya sura ya kumi na moja ya Mwanzo na pia kulingana na historia ya kilimwengu, aliazimia kutimiza mambo matatu. Alitaka kujenga taifa lenye nguvu, na akalijenga. Alitaka kueneza dini yake mwenyewe, na akaieneza. Alitaka kujifanyia jina, nalo pia akafualu. Kufaulu kwake kulikuwa kukuu sana hivi kwamba ufalme wa Babeli uliitwa kichwa cha dhahabu kati ya serikali zote za ulimwengu. Kwamba dini yake ilipata umaarufu inathibitishwa kwa ukweli kwamba Maandiko yanaitambulisha kabisa na Shetani katika Isaya Sura ya 14 na Ufunuo Sura ya 17-18. Na kwa historia tunaweza kuthibitisha ya kwamba iliuvamia ulimwengu mzima na ndiyo msingi wa kila utaratibu wa dini ya

ibada za sanamu, na kiini cha hadithi za miungu, ingawa majina ya miungu yanatofautiana katika sehemu mbali mbali za nchi kulingana na lugha ya watu. Kwamba alijifanyia jina kwa ajili yake mwenyewe na kwa wafuasi wake ni wazi, kwa kuwa mradi wakati huu wa sasa unaendelea (hadi Yesu atakapojifunua kwa ndugu Zake) yeye ataabudiwa na kuheshimiwa, ingawa itakuwa chini ya jina jingine mbali na Nimrodi, na katika hekalu ambalo ni tofauti kidogo na lile aliloabudiwa hapo awali.

Kwa kuwa Biblia haishughuliki na historia za mataifa mengine kirefu, itakuwa ni muhimu kuchunguza kumbukumbu za kale za kilimwengu kupata jibu letu la jinsi Pergamo ulivyofanyika kiti cha enzi cha dini ya Kishetani ya Babeli. Chimbukko kubwa la taarifa hiyo itakuwa katika kumbukumbu za utamaduni wa Kimisri na wa Kiyunani. Sababu yake ni hii kwamba Misri ilipata sayansi yake na hisabati zake kutoka kwa Wakaldayo nayo Uyunani ulizipata kutoka Misri.

Sasa kwa kuwa makuhani ndio waliokuwa na jukumu la kufundisha sayansi hizi, na kwa kuwa sayansi hizi zilitumiwa kama sehemu ya dini, tayari tunajua ufunguo wa vile dini ya Babeli ilivyoimarika katika nchi hizi mbili. Ni kweli pia kwamba kila wakati taifa moja lilipoweza kulishinda taifa jingine, baada ya kitambo kidogo dini ya lililoshinda ilikuja kuwa dini ya lililoshindwa. Inajulikana vizuri sana ya kwamba Wayunani walikuwa na alama zile zile za Zodiaka kama za Wababeli; na imegunduliwa katika kumbukumbu za kale za Wamisri kwamba Wamisri waliwapa Wayunani elimu yao ya miungu mingi. Hivyo siri za Babeli zilisambaa kutoka taifa moja hadi jingine mpaka zikatokea huko Rumi, Uchina, India na hata katika Marekani zote mbili ya Kaskazini na ya Kusini tunaona jambo lile lile la msingi wa kuabudu.

Historia za kale zinakubaliana na Biblia ya kwamba dini hii ya Babeli hakika kabisa haikuwa dini ya awali ya watu wa kwanza duniani. Ilikuwa ni ya kwanza kuiacha imani ya asili; lakini yenyewe haikuwa ya asili. Wanahistoria kama Wilkinson na Mallet wamethibitisha kabisa kabisa kutoka kwenye maandishi ya kale ya kwamba wakati mmoja watu wote wa duniani walimwamini MUNGU MMOJA, mwenyezi, wa milele, asiyeonekana, Ambaye kwa Neno la kinywa Chake alinena vitu vyote vikawepo, na kwamba katika tabia Yake alikuwa mwenye upendo na mwema na mwenye haki. Lakini kwa kuwa Shetani daima atapotosha cho chote awezacho, tunamwona akipotosha nia na mioyo ya watu ili kwamba waikatae ile kweli. Kwa vile daima amejitahidi apate kuabudiwa kama kwamba yeye alikuwa ndiye Mungu wala si mtumishi na kiumbe cha Mungu, aliondoa ibada kutoka kwa Mungu kwa kusudi kwamba aweze kuileta kwake mwenyewe na kwa hiyo atukuzwe. Kwa kweli hakika alitimiza shauku yake ya kusambaza dini yake kote ulimwengu mzima. Jambo hili linathibitishwa na Mungu katika Kitabu cha Warumi, "Wakati walipomjua Mungu, hawakumtukuza kama ndiye Mungu, mpaka wakapotea katika uzushi wao, na kwa mioyo yenye giza wakakubali dini iliyopotoka mpaka waliabudu viumbe wala si Muumba."

Kumbukeni, Shetani alikuwa kiumbe cha Mungu (Mwana wa Asubuhi). Hivyo tunaona ya kwamba pale ambapo wakati mmoja ukweli ulisambazwa kati ya wanadamu, na wote wakaishikilia hiyo kweli moja, kulikuja siku baadaye wakati kundi kubwa lilipomwacha Mungu na likaeneza utaratibu wa ibada za kishetani kila mahali ulimwenguni. Historia inathibitisha ya kwamba wale wa kabila la Shemu waliosimama pamoja na ukweli usiobadilika walikuwa katika upinzani thabiti dhidi ya wale wa Hamu walioiacha kweli na kujiingiza kwenye uongo wa ibilisi. Hakuna wakati wa kujiingiza katika mjadala wa jambo hili; limeingizwa tu upate kuona kulikuweko na dini mbili na mbili peke yake, na ile ya yule mwovu ikaenea kote ulimwenguni.

Imani ya Mungu mmoja iligeuka ikawa imani ya miungu mingi huko Babeli. Uongo wa ibilisi na mafundisho ya siri za ibilisi ziliinuka dhidi ya kweli ya Mungu na siri za Mungu katika mji huo. Shetani kweli akawa mungu wa dunia hii na akawashurutisha kumwabudu wale aliokuwa amewadanganya, akiwafanya waamini ya kwamba yeye alikuwa ndiye Bwana kweli.

Dini ya miungu mingi ya yule adui ikaanza na fundisho la utatu. Ilikuwa ni huko nyuma kabisa katika zamani za kale sana ambako wazo la "Mungu mmoja katika nafsi tatu" lilizaliwa. Ni ajabu vipi ya kwamba wanatheolojia wetu wa kisasa hawakuona jambo hili; lakini kwa dhahiri kama vile baba zao walivyodanganywa na Shetani, wao wangali wanaamini katika nafsi tatu katika Uungu. Hebu na tuonyeshwe mahali pamoja tu katika Maandiko ambapo pana ushuhuda wo wote kwa fundisho hilo. Je! si ni jambo la ajabu kwamba wakati uzao wa Hamu ulipoenda zake katika ibada za Kishetani ambazo zilikuwa na wazo la kimisingi la miungu mitatu kwamba hakuna dalili hata moja ya uzao wa Shemu wanaoamini jambo kama hilo ama walio na desturi za ibada zinazohusika na hata mfano wake? Sio ajabu kwamba Waebrania waliamini, "Sikia, Enyi Israeli, Bwana Mungu wenu ni Mungu MMOJA", kama kungalikuweko na nafsi tatu katika Uungu? Ibrahimu, wa mzao wa Shemu, katika Mwa. 18, aliona Mungu MMOJA tu na malaika wawili.

Sasa utatu huu ulioneshwaje? Ulioneshwa katika umbo la pembetatu zilizo sawa kama vile tu unavyooneshwa huko Rumi leo. Ajabu, Waebrania hawakuwa na wazo kama hilo. Sasa ni nani aliye sahihi? Je! Ni Waebrania au Wababeli? Huko Asia wazo la imani ya miungu mingi la miungu watatu katika mmoja lilitokea katika sanamu iliyokuwa na vichwa vitatu katika mwili mmoja. Yeye anaoneshwa kama watu watatu. Huko India, waliamua mioyoni mwao kumwonyesha kama mungu mmoja katika maumbo matatu. Sasa kwa kweli hiyo ni theolojia nzuri ya kisasa. Huko Japani kuna Budha mkuu mwenye vichwa

vitatu kama yule tuliyekwisha kuelezea.

Lakini ya wazi sana kuliko zote ni ile inayoonyesha wazo la utatu wa Mungu katika hali tatu za: 1 Kichwa cha mzee kikionyesha Mungu Baba, 2 Duara ambayo katika zile siri ilimaanisha "Mzao" ambao nao unamaanisha Mwana. 3 Mabawa na mkia wa ndege (hua). Hapa ndipo palipokuwapo na fundisho la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, nafsi tatu katika Uungu, utatu kweli-kweli. Unaweza kuona jambo lile lile huko Rumi. Sasa hebu niulize mara nyingine tena, je! hivi haishangazi kwamba ibilisi na watu wake wanaomwabudu kweli walifunuliwa ukweli mwingi zaidi ya baba wa imani (Ibrahimu) na uzao wake? Je! haistaajabishi ya kwamba waabudu Shetani, walijua mambo mengi zaidi kuhusu Mungu kuliko watoto wa Mungu? Sasa hivyo ndivyo wanatheolojia wa kisasa wanavyojaribu kutuambia wakati wanapozungumza juu ya utatu. Kumbuka tu jambo hili moja tangu sasa na kuendelea: kumbukumbu hizi ni kweli na jambo hili ni kweli_Shetani ni mwongo na baba wa uongo, na wakati wo wote anapokuja na nuru yo yote bado ingali ni uongo. Yeye ni muuaji. Na fundisho lake la utatu limeangamiza umati wa watu na litaangamiza mpaka Yesu atakapokuja.

Kulingana na historia haikuchukua muda mrefu kwa badiliko kufanywa katika wazo hili la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. Shetani aliwachukua hatua kwa hatua kutoka kwenye ile kweli. Wazo la Uungu lililojitokeza sasa lilikuwa: 1 Baba wa milele, 2 Roho wa Mungu aliyefanyika mwili katika mama wa KIBINADAMU. (Je! hilo linawafanya mfikiri?) 3 Mwana fulani wa Kiungu, tunda la huko kufanyika mwili, (Mzao wa mwanamke).

Lakini ibilisi hajatosheka. Bado hajafaulu kuabudiwa, ila kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Kwa hiyo wanachukua watu mbali zaidi kutoka kwenye kweli. Kupitia mafundisho yake ya siri yeye anawafunulia watu ya kwamba kwa kuwa yule baba Mungu mkuu asiyeonekana hajishughulishi na mambo ya kibinadamu, lakini yeye anaendelea kuwanyamazia, basi kwa sababu hiyo anaweza kuabudiwa katika ukimya. Kwa kweli hiyo inamaanisha kutomjali sana iwezekanavyo, ama kabisa. Fundisho hili lilienea duniani pia, na hata leo huko India unaweza kuona ya kwamba mahekalu ya yule muumbaji mkuu, mungu mkimya, inashangaza idadi yake ni ndogo.

Kwa kuwa halikuwa jambo la lazima kumwabudu yule muumba-baba, basi lilikuwa tu ni jambo rahisi kwamba ibada zilibadilishwa zikawa ni "Mama na Mwana" kama vitu vya kusujudiwa. Huko Misri kulikuwako na muungano huo huo wa mama na mwana walioitwa Isiri na Osiri. Huko India ilikuwa ni Isi na Iswara. (Angalia jinsi hata majina yanavyofanana.) Huko Asia ilikuwa ni Sibele na Diusi. Huko Rumi na Uyunani ikawa ni vile vile tu. Na huko China. Vema, wazia mshangao wa baadhi ya wamishenari wa Katoliki ya Kirumi walipokuwa wanaingia Uchina wakakuta huko Madona na Mwana akiwa na miali ya nuru inayotoka kutoka kwenye kichwa cha huyo mtoto mchanga. Sanamu hiyo ingeweza vizuri kubadilishwa kwa urahisi na ile iliyoko Vatikani ila kwa tofauti iliyopo katika sura ya uso.

Inatubidi sasa kugundua asili ya mama na mwana. Yule mungu-mama asili wa Babeli alikuwa ni Semirami ambaye aliitwa Rea katika nchi za mashariki. Alimshika mwana mikononi mwake, ambaye ingawa alikuwa ni mtoto mchanga, alisemekana kwamba ni mrefu, mwenye nguvu, mwenye sura nzuri na hasa sana anayewavutia wanawake. Katika Ezekieli 8:14 aliitwa Tamuzi. Kati ya waandishi wa vitabu bora sana yeye aliitwa Bakusi. Kwa Wababeli alikuwa Ninasi. Sababu ya yeye kuwakilishwa kama mtoto mchanga aliyeshikwa mikononi na hata hivyo anatajwa kama mtu mkuu na mwenye nguvu mno ni kwamba yeye anajulikana kama "Mume- Mwana". Moja ya jina lake la cheo lilikuwa ni "Mume wa Mama", na huko India ambako hao wawili wanajulikana kama yule Iswara na Isi, yeye (mume) anawakilishwa kama yule mtoto mchanga kwenye titi la mke wake mwenyewe.

Kwamba huyu Ninasi ndiye yule Nimrodi wa Biblia tunaweza kuthibitisha kwa kulinganisha historia na taarifa ya Kitabu cha Mwanzo. Pompei alisema, "Ninasi, mfalme wa Ashuri, alibadilisha njia za maisha ya kawaida ya kale kwa tamaa ya kuteka nchi. NDIYE ALIYEKUWA WA KWANZA KUFANYA VITA DHIDI YA MAJIRANI ZAKE. Alishinda mataifa yote kutoka Ashuri mpaka Libia kwa maana watu hawa hawakuwa na ujuzi wa vita." Diodoru anasema, "Ninasi alikuwa ndiye wa zamani sana wa wafalme wa Waashuri aliyetajwa katika historia. Akiwa mwenye tabia ya kupenda vita sana aliwafunza kwa ukakamavu sana vijana wengi mbinu za vita. Aliiteka Babilonia wakati hakukuweko na mji wo wote wa Babeli." Kwa hiyo tunaona jambo hili ya kwamba huyu Ninasi alianza kuwa mkuu huko Babeli, akaujenga Babeli na kuiteka Ashuri, akawa mfalme wake, kisha akaendelea kuangamiza majimbo mengine makubwa ambako watu hawakuwa na ujuzi wa vita na waliishi maisha ya kawaida kama alivyosema Pompei.

Sasa katika Mwanzo 10, ikinena juu ya ufalme wa Nimrodi inasema,

> *"Mwanzo wa ufalme wake ulikuwa Babeli na Ereku, na Akadi, na Kalne, katika nchi ya Shinari. Kutoka katika nchi hiyo akatoka Ashuri na akajenga Ninawi, na Kala nk."*

Lakini wafasiri walifanya kosa kwa kutafsiri Ashuri kama jina kwa kuwa ni kitendo, na katika Kikaldayo linamaanisha „kutia nguvu." Hivyo basi ilikuwa ni Nimrodi, ambaye baada ya kutiwa nguvu (alianzisha ufalme wake kwa kuanzisha jeshi la kwanza duniani ambalo alilifundisha kwa kulifanyiza mazoezi na kwa mazoezi magumu ya kuwinda) alienda mbele ya Shinari na jeshi lake hodari na kuyashinda mataifa na

kujenga miji kama Ninawi, ambao uliitwa kwa jina lake, kwa maana hata leo sehemu muhimu ya mabaki ya mji huo inaitwa Nimroudi!

Kwa kuwa tumegundua Ninasi alikuwa ni nani, ni muhimu sasa kugundua baba yake alikuwa ni nani. Kulingana na historia alikuwa ni Beli, aliyeuanzisha Babeli. (Sasa inapaswa kufahamika hapa ya kwamba Beli aliuanzisha kwa maana ya kwamba yeye ndiye aliyeanzisha harakati hizi zote, lakini ilikuwa ni mwanawe, Ninasi, aliyeusimamisha na ndiye aliyekuwa mfalme wa kwanza nk.) Lakini kulingana na Maandiko, baba wa Nimrodi alikuwa ni Kushi: "Na Kushi akamzaa Nimrodi." Si tu hii ni kweli bali tunaona ya kwamba Hamu alimzaa Kushi. Sasa, katika utamaduni wa Kimisri Beli aliitwa Herme, na Herme maana yake ni, "MWANA WA HAMU." Kulingana na historia Herme alikuwa nabii mkuu wa ibada za sanamu. Yeye alikuwa mfasiri wa miungu. Jina jingine aliloitwa kwalo lilikuwa ni Merkuri. (Soma Matendo 14:11-12)

Higinu anasema hivi kuhusu mungu huyo aliyejulikana kwa majina kadha kama vile Beli, Herme, Merkuri nk, "Kwa miaka mingi watu waliishi chini ya serikali ya Jove (si yule Jove wa Kirumi, lakini Yehova wa Waebrania ambaye ametangulia historia ya Kirumi) bila miji na bila sheria, na wote wakinena lugha moja. Lakini baadaye Merkuri (Beli, Kushi) alifasiri lugha za wanadamu (ambapo kutokana na chanzo hicho mfasiri anaitwa Hermeneute) mtu yuyo huyo aliyatawanya mataifa. Ndipo mizozo ikaanza." Inaonekana kutokana na jambo hili ya kwamba Beli ama Kushi, baba wa Nimrodi, hapo awali alikuwa ndiye kiongozi aliyewaongoza watu kutoka kwa Mungu wa kweli na kuwatia moyo watu kama "mfasiri wa miungu" wachukue dini ya namna nyingine. Aliwatia moyo waendelee na ule mnara ambao mwanawe kusema kweli ndiye aliyeujenga. Ushawishi huu ndio ulioleta ule mchafuko na mgawanyiko wa wanadamu, hivi kwamba yeye alikuwa yote mawili "mfasiri na mchafuaji."

Kushi, basi, alikuwa baba wa ule utaratibu wa imani ya miungu mingi na wakati watu walipofanywa miungu na watu, yeye bila shaka, akawa baba wa miungu. Sasa Kushi aliitwa Beli. Na Beli katika hadithi za miungu ya Kirumi alikuwa ni Janu. Yeye huchorwa akiwa na nyuso mbili na alibeba rungu ambayo kwayo aliwafadhaisha na "kuwatawanya" watu. Ovidi anaandika ya kwamba Janu alisema kuhusu habari zake mwenyewe "watu wa kale waliniita mimi Machafuko". Kwa hiyo tunaona ya kwamba Kushi wa Biblia, yule mwasi wa kwanza dhidi ya imani ya Mungu mmoja aliitwa Beli, Belu, Herme, Janu, nk. miongoni mwa watu wa kale. Alikusudia kuleta mafunuo na fasiri kutoka kwa miungu kwenda kwa watu. Kwa kufanya jambo hilo alisababisha ghadhabu ya Mungu kuwatawanya watu, akileta utengano na machafuko.

Sasa umbali huu tumeona ni wapi imani ya miungu mingi ama kuabudu miungu mingi kulikotoka. Lakini una habari ya kwamba pia tulipata kutajwa kwa mtu aliyeitwa Kushi ambaye alipewa cheo cha "baba wa miungu"? Umeona hapa kiini cha hoja ya kale ya hadithi za kale za miungu, ya kwamba miungu wanajitambulisha na wanadamu? Hapo ndipo ibada za mizimu zinapochimbuka. Kwa hiyo pengine hebu kidogo tuchunguze historia tupate kujua habari za ibada za mizimu. Vema, ilielezewa ya kwamba Kushi aliingiza ibada ya miungu watatu ya baba, mwana na roho. Miungu watatu ambao wote walikuwa sawa. Lakini alijua juu ya mzao wa mwanamke unaokuja, kwa hiyo hapana budi patokee mwanamke na uzao wake uingie kwenye picha. Hili lilitimizwa wakati Nimrodi alipokufa. Mkewe, Semirami alimfanya mungu, na hivyo basi akajifanya mwenyewe mama wa huyo mwana na pia mama wa miungu. (Kama vile vile tu kanisa la Kirumi lilivyomfanya Mariamu kuwa mungu. Wanadai alikuwa hana dhambi na alikuwa ni Mama wa Mungu.) Yeye (Semirami) alimwita Nimrodi "Zeroashta" ambalo linamaanisha, "uzao wa mwanamke ulioahidiwa."

Bali haikuchukua muda mrefu sana hata mwanamke huyo alipoanza kuwavutia watu kuliko mwana, na haikuchukua muda akawa ndiye aliyeoneshwa akimkanyaga yule nyoka chini ya mguu wake. Walimwita "malkia wa mbinguni" na kumfanya wa kiungu. Jinsi ilivyo sawa na siku hizi ambapo Mariamu, mama wa Yesu, ameinuliwa kufikia kutopatikana na mauti na sasa hivi kuanzia mwezi wa Septemba 1964 halmashauri ya Vatikani inajaribu kumpa Mariamu sifa zisizo zake, kwa kuwa wao wangetaka kumwita, "Mariamu Mpatanishi," "Mariamu Mama wa Waamini Wote," ama "Mama wa Kanisa." Kama kulipata kuweko na ibada za mizimu za Kibabeli katika dini, ni dini ya Kanisa la Rumi.

Si kwamba ibada ya mizimu pekee ilianzia Babeli lakini pia vivyo hivyo ibada za maumbile. Ilikuwa ni hapo Babeli miungu ilipotambulishwa na jua na mwezi, nk. Kitu muhimu sana katika maumbile kilikuwa ni jua ambalo lina asili ya kutoa nuru na joto na linaonekana kwa mwanadamu kama mpira wa moto mbinguni. Hivyo basi mungu mkuu angekuwa ni mungu jua ambaye walimwita Baali. Mara nyingi jua lilionyeshwa kama duara la mwali wa moto na mara kidogo kuuzunguka mwali huo pakatokea nyoka. Haikuchukua muda mrefu hata huyo nyoka akawa ndiye alama ya jua na mwishowe akaabudiwa. Kwa hiyo shauku ya moyo wa Shetani ikatimizwa kikamilifu. Aliabudiwa kama Mungu. Kiti chake cha enzi kiliwekwa imara. Watumwa wake walimsujudia. Kule Pergamo katika mfano wa nyoka aliye hai aliabudiwa. Ule Mti wa Kujua Mema na Mabaya, sasa ukionyeshwa katika umbo la nyoka aliye hai haukuwa tu umemdanganya Hawa bali wanadamu wengi.

Lakini Pergamo ulifanyikaje kiti cha enzi cha Shetani iwapo Babeli ndio uliokuwa kiti cha enzi? Jibu tena liko katika historia. Wakati Babeli ilipotekwa na Wamedi na Waajemi, yule kuhani-mfalme, Atalasi aliukimbia huo mji akaenda huko Pergamo pamoja na makuhani wake na mafundisho yake ya siri za

miungu. Akaanzisha ufalme wake huko nje ya himaya ya Kirumi, ndipo akafanikiwa chini ya ulinzi wa ibilisi.

Huu umekuwa muhtasari mfupi sana wa historia ya dini ya Kibabeli na kuwasili kwake Pergamo. Maswali mengi bila shaka yameachwa bila kujibiwa na mengi zaidi, hapana shaka, yangeweza kusemwa kutuangazia, lakini hili halikusudiwi kuwa somo la historia, zaidi sana linakusudiwa kuwa msaada wa kulisoma Neno.

**LAWAMA**

Ufunuo 2:14-15

> *"Lakini ninayo maneno machache juu yako, kwa kuwa unao huko watu washikao mafundisho ya Balaamu, yeye aliyemfundisha Balaki atie ukwazo mbele ya wana wa Israeli, kwamba wavile vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu, na kuzini.*
>
> *Vivyo hivyo wewe nawe unao watu wayashikao mafundisho ya Wanikolai vile vile, ambayo nayachukia."*

Katika Wakati huu wa Pergamo Bwana analaumu mafundisho mawili ambayo Yeye anayachukia: 1 Fundisho la Balaamu ambalo liliingiza ibada za sanamu na anasa za dhambi zilizopita kiasi kwa Israeli huko Baal-Peori, na 2 Fundisho la Wanikolai, ambalo lilikuwa ni matendo tu katika Wakati wa Efeso. Unganisha mashtaka haya na jambo la kwamba amekuwa akitilia mkazo Pergamo kama kiti cha enzi cha Shetani, na ni rahisi sana na ni vema kumalizia ya kwamba kwa namna fulani dini ya Babeli imechanganyikana na Ukristo.

Sasa jambo hili si la kukisia tu bali ni kweli ya kihistoria ambayo tutaithibitisha kwa kurudi katika historia kwenye kama 36 B.K. na kufikia kwenye Baraza la Nikea la 325. Wakati Wakristo (hasa Wayahudi kwa kuzaliwa) walipotawanyika kila mahali kutoka Yerusalemu walienda kila mahali wakihubiri Injili, zaidi sana katika masinagogi. Hivyo basi katika kipindi cha miaka mitatu, ama kama 36 B.K. Injili ilikuwa imepelekwa Rumi na Yunia na Androniko, ambao kulingana na Warumi 16:7 walikuwa ni mitume. Kazi ilistawi kule kwa miaka kadha wa kadha mpaka ugomvi wa sikuzote miongoni mwa Wayahudi wenyewe kwa wenyewe ulisababisha Mfalme Klaudio kuwafukuza kutoka Rumi. Wayahudi wakiwa wamefukuzwa kutoka kwenye mji huo uti wa mgongo wa kanisa hilo dogo kwa kweli ulivunjwa kabisa. Labda hata na wazee walikuwa ni Wayahudi na kwa hiyo wangekuwa wameondoka. Lile kundi litakuwa halihudumiwi na kwa kuwa Neno halikuwa limeandikwa kama mwongozo ingekuwa ni rahisi sana kwa kundi hili dogo kupeperushwa ama kusongwa na wanafalsafa na wapagani wa siku hizo. Huku mbwa mwitu wakali wakizungukazunguka, na roho ya mpinga-Kristo ikiwa imeachiliwa, twaona kutoka kwenye historia ya kwamba kanisa hili dogo hapo Rumi lilirudi nyuma vibaya kabisa, na likaanza kuingiza ibada za kipagani chini ya majina ya Kikristo.

Kwa vile kipindi cha kule kufukuzwa kilidumu miaka 13, wale waanzilishi, Yunia na Androniko hawakurudi mpaka 54 B.K. Hebu wazia hofu yao kuu walipokuta kanisa likiwa na jina la Kikristo na huku ni pagani vya kutisha. Kulikuweko na madhabahu kanisani ambapo waliweka ubani na kuadhimisha ibada za kipagani. Wale viongozi wa kanisa hilo waliojing"ang"aniza hawangeweza kuambiwa kitu, kwa hiyo pamoja na wale wachache waliokuwa wamejaribu kudumu waaminifu wakaanzisha kanisa jipya, ama Kanisa la Pili la Rumi. Mungu alitenda kazi kwa neema kati yao kwa ishara na maajabu hivi kwamba kanisa la tatu lilianzishwa. Na ingawa lile Kanisa la Kwanza lilikemewa kwa kuwa la kipagani wala SI la Kikristo katika ibada zake halikuacha jina lake lakini lilibaki na LINGALI LIMEBAKI Kanisa la Kwanza la Rumi_ Kanisa Katoliki la Kirumi.

Sasa wengi wetu sisi tuna wazo baya kwamba ye yote na wote wanaojiita Wakristo wangekuwa ndio lengo la ibilisi na kwa hiyo wao ndio wanaostahimili udhalimu wa ukatili wa serikali. Lakini sivyo. Kanisa hili la kwanza lilikuwa limeanza kusitawi na kuongezeka sana katika idadi yao hata wafalme na maafisa mbalimbali wa serikali kweli walilipendelea kanisa hilo kwa sababu za kisiasa.

Hivyo basi wakati viongozi wa Kanisa la Kwanza huko Rumi walipojikuta wanapendelewa, walichukua nafasi hiyo kuipambanisha serikali na waamini wa kweli na kudai wateswe la sivyo warudi kwenye kundi lao. Askofu mmoja kama hao wa Kanisa la Kwanza la Rumi alikuwa ni Aniseta ambaye aliishi katika karne ya pili na alikuwa hirimu wa Polikapu.

Wakati yule mtakatifu Polikapu aliposikia ya kwamba Kanisa la Kwanza la Kikristo huko Rumi lilikuwa linashiriki katika desturi za kipagani na limepotosha kweli ya Injili, yeye alienda kule kuwasihi sana wabadilike. Aliwaona wakisujudu mbele ya sanamu zilizoitwa kwa majina ya mitume na watakatifu. Aliwaona wakiwasha mishumaa na kuchoma ubani juu ya madhabahu. Aliwaona wakiendesha ibada ya Pasaka chini ya jina la Ista, ambapo waliuinua mkate wenye umbo la duara ambao ulimtukuza mungu jua, halafu wakamwaga divai kama sadaka ya kumimina kwa miungu. Lakini mtakatifu huyu mzee aliyekuwa amesafiri maili 1500 hangeweza kuzuia huko kutumbukia kwao. Mungu alinena kupitia kwake wakati tu alipokuwa anaondoka, "Efraimu amejiungamanisha na sanamu zake; mwache," Hos. 4:15. Polycarp

hakurudi tena.

Aliyemfuata Aniseta alikuwa askofu katili wa Rumi jina lake Vikta. Yeye hata aliingiza sikukuu nyingi zaidi na ibada za kipagani katika Kanisa la Kwanza, na pia akashika kujaribu awezavyo kuyashawishi makanisa ya kweli ya Kikristo kuingiza mawazo yale yale. Hawakufanya kama alivyowaomba kwa hiyo akawashawishi maafisa wa serikali kuwatesa waamini, wakifurahia kuwapeleka mahakamani, wakiwatupa gerezani na hata kuwaua wengi. Mfano kama huo wa matendo yake maovu unapatikana katika historia ambapo Mfalme Septima Severa alishawishiwa na Kalistasi (rafiki wa Vikta) kuua 7000 huko Thesalonike kwa sababu waamini hawa wa kweli waliendesha ibada ya Pasaka kulingana na Bwana Yesu wala si kulingana na ibada ya Astarte.

Tayari ule mzabibu wa uongo ulikuwa ukiachilia hasira yake dhidi ya Mungu aliye hai kwa kuwaua wateule, kama vile alivyofanya mtangulizi wake, Kaini, kumwua Habili.

Kanisa la kweli liliendelea kujaribu kulifanya Kanisa la Kwanza kutubu. Halingetubu. Liliongezeka katika ukubwa na ushawishi. Lilianzisha njama zisizo na mwisho za kuuvunjia sifa uzao wa kweli. Walidai ya kwamba wao na wao pekee ndio waliokuwa wawakilishi wa kweli wa Bwana Yesu Kristo, na kujivunia ukweli kwamba wao walikuwa kanisa la kwanza huko Rumi, na wao peke yao ndio Kanisa la Kwanza. Kweli walikuwa Kanisa la Kwanza, na KWELI NDIO Kanisa la Kwanza.

Kwa hiyo mnamo wakati wa wakati huu wa tatu wa kanisa tuna makanisa mawili yaliyokuwa na jina lile lile lakini kukiweko na tofauti ya chuki kati yao. Moja limeiacha ile kweli, likajiunga na sanamu na halina uhai ndani yake. Limejichanganya mbegu na dalili za mauti, (si uhai), zinaliandama. Lina nguvu kwa kuwa na wafuasi wengi. Linapendwa na ulimwengu. Hilo jingine ni kundi dogo linaloteswa. Lakini linafuata Neno, na ishara zinafuatana nalo. Wagonjwa wanaponywa na wafu wanafufuliwa. Liko hai kwa Uzima na Neno la Mungu. Halipendi uzima wake, lakini linashikilia Jina Lake na imani Yake hata mauti.

Na kwa hiyo yale mateso mabaya sana ya serikali ya Kirumi yaliwaangukia waamini wa kweli mpaka Konstantino alipoinuka na kutoa uhuru wa kuabudu. Inaonekana kuna sababu mbili ambazo zilifanya uhuru huu utolewe. Kwanza wafalme wengi wazuri hawakuwa wameruhusu mateso, lakini walipoaga dunia, walifuatiliwa na wale waliowaua Wakristo. Yalikuwa hayana sababu hivi kwamba watu hatimaye wakaona kwamba Wakristo wanapaswa kuachwa peke yao. Sababu ya pili na inayojulikana sana ni kwamba Konstantino alikuwa na vita vigumu sana mbele yake katika kuitawala dola yake. Usiku mmoja katika ndoto aliona msalaba mweupe ukijitokeza mbele yake. Aliona kwamba hii ilikuwa ni bahati nzuri kwake ya kwamba kama Wakristo wakiomba apate ushindi, angeshinda vita. Aliwaahidi uhuru endapo angeshinda. Alishinda na uhuru wa kuabudu ukatolewa katika azimio la Nante la mwaka wa 312 B.K.

Lakini uhuru huu wa kutokana na mateso na kuuawa haukuwa wa haki kama vile ulivyoonekana kwanza. Konstantino sasa ndiye aliyekuwa mwangalizi. Kama mwangalizi kuhusika kwake kulikuwa kwa namna fulani zaidi ya mtazamaji, kwa kuwa aliamua ya kwamba kanisa lilihitaji msaada wake katika shughuli zake. Alikuwa amewaona wakibishania mambo mbalimbali, moja ya hayo lilimhusu Ariasi, Askofu wa Alekizanda, aliyewafundisha wafuasi wake ya kwamba Yesu hakuwa kwa kweli ni Mungu lakini alikuwa kiumbe cha chini kidogo, akiwa ameumbwa na Mungu. Kanisa la Magharibi lilishikilia mawazo tofauti, likiamini ya kwamba Yesu alikuwa nafsi halisi ya Mungu na kama walivyosema, „sawasawa na Baba“. Kukiweko na mambo kama hayo, pamoja na kupenyeza kwa ibada za kipagani katika ibada, mfalme aliitisha Baraza la Nikea katika mwaka wa 325 akiwa na wazo kwamba angeyaleta makundi yote pamoja mahali ambapo wangetatua tofauti zao, na wafikie uelewano wa pamoja, na wote wawe mmoja. Je! si ni la ajabu kwamba ingawa jambo hili lilianza na Konstantino halikufa lakini lingali hai kabisa leo kama ”Baraza la Makanisa Ulimwenguni“? Na mahali aliposhindwa kufanikiwa kweli katika jambo hilo, litafanikiwa katika siku hii kupitia kwenye harakati za ekumenia.

Sasa huku kuingilia kati kwa serikali katika kanisa ni jambo la kijinga kwa maana ulimwengu haufahamu aidha kweli inayopatikana katika Neno ama njia za kanisa. Mbona, uamuzi ule hasa uliotolewa na baraza hilo ya kwamba Ariasi alikuwa amekosea ulibadilishwa miaka miwili baadaye na mfalme na kwa miaka mingi fundisho hilo la uongo liliingizwa kwa hila na watu.

Lakini kwamba kanisa na serikali vingeungana kwa kweli ilijulikana kabla na Bwana. Jina lenyewe hasa Pergamo linamaanisha “kuolewa kwelikweli”. Na kwa kweli serikali na kanisa vilifunga ndoa; siasa na dini viliungana. Watoto wa muungano huo wamekuwa machotara wabaya sana walio thabiti ambao ulimwengu ulipata kuona. Kweli haimo ndani yao, lakini njia zote mbovu za Kaini (yule chotara wa kwanza) zimo.

Si kwamba tu serikali na kanisa vilifunga ndoa katika kipindi cha wakati huu, lakini ile dini ya Babeli iliunganishwa rasmi na Kanisa la Kwanza. Shetani sasa alikuwa na njia ya kulifikia Jina la Kristo na alitawazwa kama Mungu katika ibada. Kwa msaada wa mali za serikali ya dola makanisa yalirithi majengo mazuri yaliyojaa madhabahu za marmar nyeupe na vinyago vya watakatifu waliokufa. Na papa hapa katika wakati huu ndipo yule “mnyama wa Ufu. 13:3 aliyepata jeraha la mauti: (Dola ya kipagani ya Kirumi) alipofufuka na kurudi kwenye utawala kama ”Dola Takatifu ya Kirumi.“ Rumi kama taifa la kidunia ilikuwa imefilisika sana na muda si muda ingefilisika kabisa; lakini haikuleta tofauti yo yote sasa, kwa

kuwa dola yake ya kidini ingeliidumisha kuwa kileleni juu ya ulimwengu ikitawala kutoka ndani ambamo haitaonekana ikifanya jambo hilo kwa nje.

Hebu niwaonyeshe kweli halisi ya Maandiko ya jambo hili, kwa kuwa sitaki mtu ye yote afikirie kwamba ninatoa ufunuo wangu mwenyewe_ule usiopatikana katika Maandiko.

Danieli 2:31-45,

> *"Wewe Ee Mfalme, uliona, na tazama, sanamu kubwa sana. Sanamu hii, iliyokuwa kubwa sana, na mwangaza wake mwingi sana, ilisimama mbele yako; na umbo lake lilikuwa lenye kutisha.*
>
> *Na sanamu hii, kichwa chake kilikuwa ni cha dhahabu safi; kifua chake na mikono yake ni ya fedha; tumbo lake na viuno vyake ni vya shaba; miguu yake ni ya chuma; na nyayo za miguu yake nusu ya chuma na nusu ya udongo.*
>
> *Nawe ukatazama hata jiwe likachongwa bila kazi ya mikono, nalo jiwe hilo likaipiga sanamu miguu yake, iliyokuwa ya chuma na udongo, likaivunja vipande vipande.*
>
> *Ndipo kile chuma, na ule udongo, na ile shaba, na ile fedha, na ile dhahabu, vilivunjwa vipande vipande pamoja, vikawa kama makapi ya viwanja vya kupepetea wakati wa hari; upepo ukavipeperusha, hata pasionekane mahali pake; na lile jiwe lililoipiga hiyo sanamu likawa mlima mkubwa, likaijaza dunia yote.*
>
> *Hii ndiyo ile ndoto, nasi tutaihubiri tafsiri yake mbele ya mfalme.*
>
> *Wewe, Ee mfalme, u mfalme wa wafalme, na Mungu wa mbinguni amekupa ufalme, na uwezo, na nguvu, na utukufu;*
>
> *Na kila mahali wakaapo wanadamu, wanyama wa kondeni na ndege wa angani amewatia mkononi mwako, Naye amekumilikisha juu ya hao wote; wewe u kichwa kile cha dhahabu.*
>
> *Na baada ya zamani zako utainuka ufalme mwingine, mdogo kuliko wewe; na ufalme mwingine wa tatu wa shaba, utakaoitawala dunia yote.*
>
> *Na ufalme wa nne utakuwa na nguvu mfano wa chuma; kwa maana chuma huvunja vitu vyote na kuvishinda; na kama chuma kisetavyo vitu hivi vyote, ndivyo utakavyovunja-vunja na kuseta.*
>
> *Na kama vile ulivyoziona hizo nyayo za miguu na vidole vyake, kuwa nusu udongo wa mfinyanzi, na nusu chuma, ufalme ule utakuwa ufalme uliogawanyika; lakini ndani yake zitakuwako nguvu za chuma, kama vile ulivyoona kile chuma kimechanganyika na udongo wa matope.*
>
> *Na kama vidole vya zile nyayo vilivyokuwa nusu chuma na nusu udongo, kadhalika ufalme ule utakuwa nusu yake una nguvu, na nusu yake umevunjika.*
>
> *Na kama vile ulivyokiona kile chuma kimechanganyika na udongo wa matope, watajichanganya nafsi zao kwa mbegu za wanadamu; lakini hawatashikamana kama vile chuma kisivyoshikamana na udongo.*
>
> *Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele.*
>
> *Na kama vile ulivyoona ya kuwa jiwe lilichongwa mlimani bila kazi ya mikono, na ya kuwa lilivunja-vunja kile chuma, na ile shaba, na ule udongo, na ile fedha, na ile dhahabu; basi Mungu aliye mkuu amemjulisha mfalme mambo yatakayokuwa baadaye; na ndoto hii ni ya hakika, na tafsiri yake ni thabiti."*

Hapa yamefunuliwa matokeo halisi ya siku zijazo, historia isiyojazwa iliyotabiriwa kuja juu ya nchi tokea wakati wa Danieli mpaka Yesu atakapokuja na kutawala kama Mwana wa Daudi. Unajulikana kama "Majira ya Mataifa." Ndani yake mlikuwemo na sehemu nne zilizogawanyika za kihistoria zilizojulikana kwa ufalme ule uliotawala katika kila sehemu: Wababeli, Waamedi na Waajemi, wa Kiyunani, wa Kirumi.

Ufalme uliokuwa mkuu sana wa zote na wenye amri zote ulikuwa wa Babeli ambao uliwakilishwa na kichwa cha dhahabu.

Uliofuatia katika utukufu ulikuwa ni wa Wamedi na Waajemi ambao kama vile historia inavyoonyesha kweli ulikuwa umepungua katika utukufu na uliwakilishwa na kifua na mikono ya fedha.

Ndipo ukafuata wakati wa Kiyunani ambao mfalme wake alikuwa kiongozi mkuu sana na hodari sana wa viongozi wote wa kijeshi ambao ulimwengu umepata kujua kwa hiyo uliwakilishwa vizuri kwa tumbo na viuno vya shaba. Ulikuwa umepungukiwa na utukufu kuliko zile nyingine zilizoutangulia.

Hatimaye ukaja ule ufalme wa mwisho ambao ulikuwa ni Dola ya Kirumi iliyowakilishwa na miguu na nyayo. Lakini ambapo hizo nyingine zilizopita ziliwakilishwa na madini safi (dhahabu safi, fedha na shaba) dola hii ya mwisho ilikuwa tu chuma safi tu kwenye miguu yake, kwa maana ilipofikia kwenye nyayo ilikuwa ni mchanganyiko wa chuma na udongo, na madini na udongo havichangamani hata na kufanya kitu thabiti na chenye nguvu. Lakini si kwamba jambo hili tu ni kweli, lakini jambo la kushangaza sana, dola hii ya mwisho (ya Kirumi) ingedumu katika hali yake ya „kuchanganyikana" mpaka wakati atakaporudi Yesu.

Dola hii ya Kirumi ya chuma (chuma kikiwakilisha nguvu na uweza mkuu wa nguvu za maangamizi dhidi ya wapinzani) ilikuwa ifanywe kwa sehemu mbili muhimu. Na kweli ilikuwa hivyo kwa kuwa hiyo dola kweli iligawanyika katika sehemu mbili—Mashariki na Magharibi. Zote mbili zilikuwa na nguvu sana, zikivunja vunja vitu vyote mbele zake.

Lakini kama ilivyo kwamba utukufu na nguvu za dola zote hupungua, vivyo hivyo dola hii ilianza kuanguka pia. Kwa hiyo Rumi ilianguka. Himaya ya Rumi ya kipagani haikuwa chuma tena. Ilivunjika-vunjika. Ilipigwa jeraha la mauti. Rumi sasa haikuweza kutawala. Ilikuwa imekwisha kabisa. Ndivyo ulimwengu ulivyodhani. Lakini jinsi ulimwengu ulivyokosea, kwa maana kichwa hicho (Rumi) ingawa kilikuwa kimetiwa jeraha lakini halikuwa la mauti. (Fasiri ya Wuest, ya Ufu. 13:3, "Na moja ya kichwa chake kilionekana kama kimetiwa jeraha la mauti, baada ya kukatwa koo. Na jeraha lake la mauti lilipona. Na ulimwengu mzima ukamfuata huyo Mnyama Mwitu katika mshangao.")

Watu huiangalia Rumi. Wanaliangalia taifa la Italia. Nao wanapotazama hawatambui ya kwamba Rumi pamoja na mipaka yake halisi ambapo papa ana eneo halisi kama milki yake kweli ni taifa ndani ya taifa, naye ana mabalozi na anapokea mabalozi. RUMI YA PAPA YA UKRISTO WA UONGO (hata unaitwa mji wa milele—jinsi lilivyo la kukufuru) SASA INATAWALA KWA DINI KWA UHODARI HATA NA ZAIDI KULIKO WAKATI DOLA YA KIPAGANI YA RUMI ILIPOTAWALA KWA NGUVU TUPU ZA CHUMA. Rumi ilihuishwa upya wakati Konstantino alipounganisha kanisa na taifa na kuimarisha muungano huo kwa kutumia nguvu. Ile roho iliyoendesha Rumi ya kipagani ndiyo roho ile ile inaongoza Rumi ya Kikristo ya uongo. Unaweza kuona jambo hilo ni kweli kwa sababu sasa unajua ya kwamba ule ufalme wa nne haukwisha; ulibadilisha tu umbo lake la nje.

Mara Baraza la Nikea lilipoelekeza nguvu za Rumi ya kisiasa kwa kanisa, ilionekana ya kwamba hapakuwepo na mipaka kwa Kanisa hili la Kwanza la Kikristo ko kote lingeenda. Hilo jina, Mkristo, ambalo hapo awali lilisababisha mateso, sasa likawa ndilo jina la watesi. Wakati huu ndio ambapo Agostino wa Hipo (354-430) alipokuwa ameanzisha kanuni kwamba kanisa linapaswa na HALINA BUDI kutumia nguvu kama ni lazima kuwarudisha watoto wake kwenye kundi, na ya kwamba ilikuwa inakubaliana na Neno la Mungu kuwaua wazushi na wakana dini. Katika mabishano yake na Wadonati yeye aliandika..." Kwa kweli ni afadhali kwamba watu waongozwe kumwabudu Mungu kwa mafundisho kuliko wasukumiwe jambo hilo kwa hofu ya adhabu ama uchungu wa maumivu, lakini hiyo si kusema ya kwamba kwa sababu kufundisha kunaleta watu bora zaidi, hivyo basi hao ambao hawatakubaliana na jambo hilo watupiliwe mbali. Kwa kuwa watu wengi wameona faida (kama tulivyokwisha kuthibitisha na tunathibitisha kila siku kwa ujuzi halisi) katika kushurutishwa kwanza kwa hofu ama maumivu, ili kwamba baadaye wapate kushawishiwa kwa mafundisho, ili kwamba wapate kufuata katika kitendo yale waliyokwisha kujifunza katika neno...ingawa hao wanaoongozwa vizuri kwa upendo ni bora zaidi, bila shaka ni wengi zaidi hao wanaosahihishwa kwa hofu. Kwa maana ni nani anayeweza kutupenda zaidi ya Kristo, Ambaye alitoa uhai Wake kwa ajili ya kondoo?

Hata hivyo baada ya kuwaita Petro na mitume wengine kwa maneno Yake peke yake, wakati alipokuja kumwita Paulo, Yeye hakumshurutisha tu kwa sauti Yake, bali hata alimtupa ardhini kwa nguvu Zake; na ili kwamba apate kumleta kwa nguvu yule anayejichafua katika giza la kukataa imani, apate kuitamani nuru ya moyo, Yeye kwanza alimpiga kwa upofu wa macho ya kimwili. Kwa nini basi Kanisa lisitumie nguvu katika kuwashurutisha wanawe waliopotea kurudi? Bwana Mwenyewe alisema, „Toka nje uende barabarani na mipakani ukawashurutishe kuingia ndani." Kwa sababu hii kama mamlaka hiyo ambayo Kanisa imepokea kwa agizo la kiungu katika wakati wake, kwa tabia ya kidini na imani ya wafalme, kuwa ndicho chombo ambacho hao wanaopatikana barabarani na mipakani—hiyo ni kusema katika uzushi wa dini na waliojitenga—watalazimishwa kuingia ndani, basi hebu na wasione vibaya wakishurutishwa."

Kiu ya damu ilikuwa inaongezeka sana. Ule mzabibu wa uongo huko Hispania sasa ulimshawishi Mfalme Makzima kujiunga nao katika kuwapiga vita waamini wa kweli ambao walikuwa na Neno na ishara na maajabu. Hivyo basi baadhi ya Waprisila waliletwa Treves na Askofu Ithakasi (385). Yeye aliwashtakia uchawi na uzinzi na wengi waliuawa. Martin wa Tours, na Ambrose wa Milan walipinga jambo hili, na wakawasihi bila kuambulia kitu ili kwamba mateso yale yakomeshwe. Wakati mateso yale yalipoendelezwa

maaskofu hawa wawili walikataa kuwa na ushirika na askofu Haidatusi na wengine walio kama yeye. Ajabu ni kwamba Baraza la Maaskofu huko Treves liliidhinisha hayo mauaji.

Tangu wakati huu na kuendelea, hasa sana kupitia katika zile Zama za Giza, tutawaona wana wa kimwili wakiwatesa na kuwaangamiza wana wa Roho, ingawa wote wawili wanadai wana Baba mmoja kama vile tu ilivyokuwa kwenye kisa cha Ishmaeli na Isaka. Lile giza la upotovu wa kiroho litaongezeka na nuru ya kweli ya Mungu itafifia mpaka kiidadi itaendelea kumeka kwa udhaifu sana. Hata hivyo ahadi ya Mungu itadumu ya kweli, "Nuru huangaza gizani wala giza haliwezi kufanya jambo lo lote juu yake."

Sasa hadi kufikia wakati huu sijaelezea jambo lile katika historia ambalo niliahidi kuzungumzia, yaani, kule kuchanganyikana kwa dini ya Nimrodi na dini ya Kikristo. Mtakumbuka ya kwamba Atalasi alikimbia toka Babeli kwenda Pergamo na kuanzisha ufalme Wake nje ya mipaka ya Dola ya Kirumi. Ufalme wake ulifanikiwa kwa miaka mingi, ukilelewa na mungu wa dunia hii. Mfululizo wa makuhani_wafalme uliendelea baada ya Atalasi mpaka kwenye utawala wa Atalasi wa III wakati ambapo kwa sababu zinazojulikana tu katika mamlaka ya Mungu akausalimisha huo ufalme kwa Rumi. Basi Juliasi Kaisari akatwaa falme hizo zote mbili ule wa kimwili na wa kiroho pia kwa kuwa yeye aliitwa sasa Kuhani Mkuu Makzima wa dini ya Babeli na kwa hiyo alikuwa kuhani-mfalme. Cheo hiki kiliendelea kwa wafalme waliomfuata mpaka ukafikia wakati wa Makzima wa III ambaye alikikataa. Kulingana na Historia ya Steven ikawa basi hapo ndipo papa alipochukua uongozi uliokataliwa na mfalme huyo na mpaka leo kungali kuna kuhani mkuu ulimwenguni, na yeye kwa kweli ni Kuhani Mkuu Makzima. Yeye huvaa taji yenye sehemu tatu na anaishi Rumi. Na katika Ufu. 17 Mungu hataji tena Pergamo kama kiti cha enzi cha Shetani wala hasemi ya kwamba huko ndiko anakoishi Shetani. La, chumba cha kiti cha enzi hakiko tena huko Pergamo, bali ni Babeli ya SIRI. Hakiko huko Babeli bali ndani ya Babeli wa SIRI. Kiko kwenye mji uliojengwa juu ya milima saba. Kiongozi wake ni mpinga-Kristo kwa kuwa amepachukua mahali pa Kristo Ambaye Ndiye pekee mpatanishi na Ambaye pekee anaweza kusamehe dhambi. Naam, Kuhani Mkuu Makzima yuko pamoja nasi leo.

**FUNDISHO LA WANIKOLAI**

Ufunuo 2:15,

> *"Vivyo hivyo wewe nawe unao watu wayashikao mafundisho ya Wanikolai, ambayo ninayachukia vile vile."*

Utakumbuka ya kwamba nilielezea katika Wakati wa Efeso kuwa lile neno, Nikolai, linatokana na maneno mawili ya Kiyunani: Nikao ambalo linamaanisha kutiisha, na Lao ambalo linamaanisha washirika. Nikolai maana yake ni, "kuwatiisha washiriki." Sasa kwa nini hili ni jambo baya sana? Ni baya kwa sababu Mungu hajaliweka kamwe kanisa Lake mikononi mwa viongozi waliopigiwa kura wanaoongozwa na mawazo ya kisiasa. Ameliweka kanisa Lake katika ulinzi wa watu waliochaguliwa na Mungu, waliojazwa Roho, watu wanaoliishi Neno na kuwaongoza watu kwa kuwalisha Neno. Yeye hajawatenganisha watu katika madaraja hivi kwamba umati uongozwe na ukasisi mtakatifu. Ni kweli ya kwamba uongozi lazima uwe mtakatifu, lakini pamoja na hayo inapasa kusanyiko lote liwe takatifu. Isitoshe, hakuna mahali katika Neno ambapo makasisi ama wahudumu ama watu wa namna hiyo hupatanisha kati ya Mungu na watu, wala hakuna mahali ambapo wanatenganishwa katika kumwabudu kwao Bwana. Mungu anataka wote wampende na kumtumikia pamoja. Unikolai huharibu amri hizo na badala yake huwatenganisha wahudumu na watu na kuwafanya viongozi wawe mabwana-watawala badala ya kuwa watumishi.

Sasa fundisho hili kweli lilianza kama tendo katika wakati wa kwanza. Yaonekana kwamba shida ilikuwa katika maneno mawili; "wazee wa kanisa" (makasisi) na "wachungaji" (maaskofu). Ingawa Maandiko yanaonyesha kwamba kuna wazee kadha wa kadha katika kila kanisa, baadhi ya watu walianza (miongoni mwao akiwemo Ignatio) kufundisha kuwa wazo la askofu lilikuwa kwamba yeye ni mtu mwenye cheo kikubwa ama mwenye mamlaka na amri juu ya wazee.

Sasa ukweli wa mambo ni kwamba neno "mzee" linaonyesha mtu huyo ni nani, ambapo neno "askofu" linaonyesha huduma ya mtu yuyo huyo. Mzee ni mtu mwenyewe. Mzee ni mtu mwenyewe. Askofu ni huduma ya huyo mtu. "Mzee" sikuzote limekuwa na kila mara litakuwa tu likimaanisha umri wa mtu katika Bwana. Yeye ni mzee, si kwa sababu amechaguliwa kwa kura ama amewekewa mikono, nk., bali ni kwa sababu yeye ana umri mkuu ZAIDI. Yeye amekolea zaidi, amefundishwa, si mwanafunzi, ni mtu anayetumainiwa kwa sababu ya ujuzi na uthabiti wa ujuzi wake wa Kikristo wa siku nyingi.

Bali sivyo, maaskofu hawakushikilia nyaraka za Paulo, bali walipendelea kwenda kwenye taarifa ya Paulo ya wakati alipowaita wazee kutoka Efeso kwenda Mileto katika Matendo 20. Katika kifungu cha 17 taarifa hiyo inasema, "wazee" waliitwa na baadaye katika kifungu cha 28 wanaitwa waangalizi (maaskofu). Nao hawa maaskofu, (bila shaka wakiwa na mawazo ya kisiasa na wenye shauku ya kutaka madaraka) walisisitiza ya kwamba Paulo alikuwa akimaanisha kuwa "waangalizi" walikuwa ni zaidi ya mzee wa mtaa ambaye ana mamlaka rasmi katika kanisa lake mwenyewe tu. Kwao askofu alikuwa sasa mtu mwenye mamlaka juu ya viongozi wengi wa mitaa. Wazo kama hilo halikuwa la Kimaandiko wala la kihistoria, hata hivyo hata mtu wa hadhi kama ya Polikapu aliegemea kwenye mwongozo kama huo.

Kwa hiyo, lile lililoanza kama tendo katika wakati wa kwanza lilifanywa fundisho la kweli na ndivyo lilivyo sasa. Maaskofu wangali wanadai mamlaka ya kuwaongoza watu na kuwatendea vile wapendavyo, wakiwaweka mahali wao wapendapo katika huduma. Jambo hili linakaidi uongozi wa Roho Mtakatifu aliyesema, "Nitengeeni Paulo na Barnaba kwa kazi ile niliyowaitia." Hili ni pinga-Neno na ni pinga-Kristo.

Mathayo 20:25-28,

*"Lakini Yesu akawaita, akasema, Mwajua ya kuwa wakuu wa Mataifa huwatawala kwa nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha.*

*Lakini haitakuwa hivyo kwenu; bali mtu ye yote anayetaka kuwa mkubwa kwenu, na awe mtumishi wenu;*

*Na mtu ye yote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu;*

*Kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi Yake iwe fidia ya wengi."*

Mathayo 23:8-9,

*"Bali ninyi msiitwe Rabi, maana Mwalimu wenu ni Mmoja, yaani Kristo; nanyi nyote ni ndugu. Wala msimwite mtu baba duniani; maana Baba yenu ni Mmoja, Aliye wa mbinguni."*

Ili kueleza jambo hili kwa wazi zaidi, hebu nielezee Unikolai kwa njia hii.

Mnakumbuka ya kwamba katika Ufunuo 13:3 inasema,

*"Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti, na pigo lake la mauti likapona. Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule."*

Sasa twajua kwamba kile kichwa kilichojeruhiwa kilikuwa ni Dola ya kipagani ya Kirumi, lile taifa kuu la dunia la kisiasa. Kichwa hiki kiliinuka tena kama "Dola ya kiroho ya Katoliki ya Kirumi." Sasa angalia jambo hili kwa makini. Ni jambo gani ililofanya Rumi ya kipagani ya kisiasa ambalo lilikuwa ndilo msingi wa mafanikio yake? Hiyo, "iligawanya na kushinda." Hiyo ndiyo iliyokuwa mbegu ya Rumi—tenganisha upate kushinda. Meno yake ya chuma yalirarua na kuangamiza. Yule aliyemrarua na kumwangamiza hangeweza kuinuka tena kama ule wakati alipoiangamiza Kathago na kutapanya chumvi humo. Mbegu zile zile za chuma zilibaki ndani yake wakati ilipoinuka kama kanisa la uongo, na mbinu zake zingali ni zile zile—tenganisha upate kushinda. Huo ni Unikolai na Mungu anauchukia.

Sasa ni jambo la kweli kihistoria linalojulikana sana kwamba wakati kosa hili lilipopenya likaingia kanisani, watu walianza kushindania huduma ya uaskofu na matokeo ikawa kwamba cheo hiki kilikuwa kikipewa wenye elimu zaidi na waliopiga hatua katika kupata mali na wenye mwelekeo wa kisiasa. Maarifa ya wanadamu na taratibu zake vikaanza kuchukua nafasi ya hekima ya Kiungu, na Roho Mtakatifu hakuwa tena anaongoza. Jambo hili bila shaka lilikuwa uovu wa kufisha, kwa kuwa maaskofu walianza kushikilia kuwa haikuhitaji tena tabia safi ya Ukristo kuhudumu aidha Neno au kuendeleza utaratibu wa dini kanisani kwa kuwa jambo muhimu ni sakramenti na taratibu zake. Jambo hili liliruhusu watu waovu (wadanganyifu) wawararue kondoo.

Pamoja na mafundisho yaliyobuniwa na wanadamu ya kuwainua maaskofu hadi mahali ambapo hawakupewa katika Maandiko, hatua iliyofuata ilikuwa ni kutoa madaraja ambayo yaliunda serikali ya kidini; kwani muda si muda palikuwepo na maaskofu wakuu juu ya maaskofu na makadinali juu ya maaskofu wakuu na hata kufikia wakati wa Bonifasi wa tatu palikuwepo na papa juu ya wote, Kuhani Mkuu.

Huku yakiwemo mafundisho ya Wanikolai na muungano wa Ukristo na Ubabeli matokeo halisi kwa jumla hayana budi yalikuwa yale Ezekieli aliyoona katika Sura ya 8:10,

*"Basi nikaingia, nikaona; na tazama, kila namna ya wadudu, na wanyama wachukizao, na taswira za vinyago vyote vya nyumba ya Israeli, zimepigwa ukutani pande zote."*

Ufunuo 18:2,

*"Akalia kwa sauti kuu, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu; umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza, kwa kuwa mataifa yote wamekunywa mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake."*

Basi fundisho hili la Wanikolai, sheria hii iliyoanzishwa kanisani haikukubalika vizuri sana kwa watu wengi kwa kuwa waliweza kusoma waraka adimu au insha juu ya Neno lililoandikwa na mtu fulani mcha mungu. Kwa hiyo kanisa lilifanya nini? Liliwafukuza walimu wenye haki na kuyachoma moto magombo. Wakasema, "Inatakiwa elimu maalum kusoma na kulielewa Neno. Mbona hata Petro alisema kwamba

mambo mengi aliyoandika Paulo yalikuwa magumu kuyaelewa." Baada ya kuliondoa Neno kutoka kwa watu, muda si muda ilifikia mahali ambapo watu kusikiliza tu yale aliyosema kasisi, na kufanya aliyowaambia. Waliyaita hayo Mungu na Neno Lake takatifu. Waliyatwaa mawazo na maisha ya watu na kuwafanya wao watumwa wa ukasisi mdhalimu.

Basi kama ukitaka uhakika kuwa Kanisa Katoliki hudai maisha na mawazo ya watu, hebu sikiliza amri ya Theodosio wa X. *Amri ya Kwanza ya Theodosio.*

Amri hii ilitolewa mara tu baada ya yeye kubatizwa na Kanisa la Kwanza la Rumi. "Sisi watawala watatu wa dola tunaamuru ya kwamba raia wetu washike kwa uthabiti dini waliyofundishwa Warumi na Mt. Petro, ambayo imehifadhiwa kwa uaminifu kwa mapokeo na ambayo sasa inatangazwa na kuhani mkuu, Damasasi wa Rumi, na Petro, askofu wa Alekizandria, mtu mwenye utakatifu wa Kimitume kulingana na msingi wa Mitume, na mafundisho ya Injili; haya na tuamini katika Uungu mmoja wa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, wenye utukufu ulio sawa katika Utatu Mtakatifu. Tunaamuru ya kwamba wanaoishika imani hii waitwe Wakristo Wakatoliki; tunawabandika wafuasi wote wasio na akili wa dini nyingine jina lenye sifa mbaya la wazushi, na kukataza mikutano yao ya nyumbani kuitwa kwa majina ya makanisa. Mbali na hukumu ya haki ya kiungu, lazima wapatilizwe kwa adhabu kali ambayo serikali yetu, ikiongozwa na hekima ya mbinguni itaamua wanastahili kupewa..."

Zile sheria kumi na tano za adhabu ambazo mtawala huyu alizotoa katika miaka mingi kama hiyo ziliwanyang"anya wale wote wanaoamini katika wokovu haki zote za kuendeleza dini yao, ziliwaondoa kwenye kazi zote za serikali, na kuwatishia faini, kuwanyang"anya mali zao, kuhamishwa na hata katika matukio fulani, kifo.

Unajua nini? Tunaelekea kabisa upande huo leo.

Kanisa Katoliki la Kirumi hujiita kanisa Mama. Linajiita kanisa la kwanza ama kanisa la awali. Hilo ni sahihi kabisa. Lilikuwa ndilo Kanisa asili la Kwanza la Rumi lililoanguka na kuingia dhambini. Lilikuwa la kwanza ambalo liliunda madhehebu. Ndani yake mlionekana matendo na baadaye mafundisho ya Unikolai. Hakuna mtu atakayekana kuwa ndilo mama. Hilo ni mama na limezaa mabinti. Sasa binti hutokana na mwanamke. Mwanamke aliyevaa vazi la rangi nyekundu anaketi kwenye vilima saba vya Rumi. Yeye ni kahaba na amezaa mabinti. Mabinti hao ni makanisa ya Kiprotestanti yaliyotoka kwake na kisha yakarudi moja kwa moja kwenye madhehebu na Unikolai. Mama huyu wa makanisa binti anaitwa kahaba. Huyo ni mwanamke ambaye hakuwa mwaminifu kwa nadhiri zake za ndoa. Aliolewa na Mungu halafu akaenda kufanya uasherati na ibilisi na katika uasherati wake amezaa mabinti walio kama yeye kabisa. Muungano huu wa mama na binti ni upinga-Neno, upinga- Roho na kwa sababu hiyo ni upinga-Kristo. Naam, UPINGA- KRISTO.

Basi kabla sijaendelea mbali sana ninataka kusema kwamba hawa maaskofu wa mwanzoni walidhani ya kwamba wao walikuwa wako juu ya Neno. Waliwaambia watu kwamba wao waliweza kuwasamehe dhambi zao wakiziungama. Hilo halikuwa kweli kamwe. Walianza kuwabatiza watoto wachanga katika karne ya pili. Kwa kweli walibatiza kwa ajili ya kuzaliwa mara ya pili. Si ajabu watu leo hii wamechanganyikiwa. Ikiwa walikuwa wamechanganyikiwa namna hiyo wakati huo, karibu sana na Pentekoste, sasa wako katika hali mbaya zaidi kuliko nyakati zote zilizopita, wakiwa umbali wa yapata miaka 2,000 kutoka kwenye ile kweli ya asili.

Loo! Kanisa la Mungu, kuna tumaini moja tu. Rudi kwenye Neno na ukadumu nalo.

## FUNDISHO LA BALAAMU

Ufunuo 2:14,

> *"Unao huko watu washikao mafundisho ya Balaamu, yeye aliyemfundisha Balaki atie ukwanzo mbele ya wana wa Israeli, kwamba wavile vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu, na kuzini."*

Sasa, huwezi kuanzisha mpango wa Unikolai kanisani na ukose pia kujiingiza kwa fundisho hili jingine. Mnaona, ukiliondoa Neno la Mungu na kazi za Roho kama njia ya kuabudia (wao wanaoniabudu Mimi yawapasa waniabudu katika Roho na kweli) basi itakulazimu uwape watu aina nyingine ya ibada kuwa kibadala, na badilisho humaanisha Ubalaamu.

Endapo tutafahamu fundisho la Balaamu ni nini katika kanisa la Agano Jipya ni heri turudi nyuma tuone lilikuwa ni nini katika kanisa la Agano la Kale na kulitumia katika huo wakati wa tatu na halafu kulileta hadi siku hizi.

Hadithi hiyo inapatikana katika Hesabu Sura za 22 hadi 25. Sasa tunajua kwamba Israeli walikuwa watu waliochaguliwa na Mungu. Walikuwa ndio Wapentekoste wa siku yao. Walikuwa wamekimbilia chini ya damu, wote walikuwa wamebatizwa katika Bahari ya Shamu nao wakatoka majini wakiimba katika Roho na kucheza kwa nguvu za Roho Mtakatifu, huku Miriamu, nabii mke, akipiga tari lake. Naam, baada

ya wakati fulani wa kusafiri hawa wana wa Israeli walifika Moabu. Mnakumbuka Moabu alikuwa ni nani. Yeye alikuwa mwana wa Lutu kwa mmoja wa mabinti wake mwenyewe aliozaa, naye Lutu alikuwa mpwawe Ibrahimu, kwa hiyo Israeli na Moabu walikuwa ni wa ukoo mmoja. Ninawatakeni mwone jambo hilo. Wamoabu waliujua ukweli, kama waliuishi au la.

Kwa hiyo Israeli wakaja hadi mipakani mwa Moabu na wakatuma wajumbe kwa mfalme wakisema, "Sisi ni ndugu. Turuhusuni tupite katika nchi yenu. Kama watu wetu au wanyama wetu wakinywa ama wakila cho chote, tutakilipa kwa moyo mweupe." Lakini Mfalme Balaki alihangaika sana. Kiongozi huyo wa kundi hilo la Wanikolai hakuwa tayari kuachilia kanisa lipite likiwa na ishara zake na maajabu na madhihirisho mabalimbali ya Roho Mtakatifu, huku nyuso zao ziking"aa kwa utukufu wa Mungu. Ilikuwa ni hatari sana, kwa kuwa huenda angepoteza baadhi ya kundi lake. Kwa hiyo Balaki alikataa kuwaruhusu Israeli wapite. Kwa kweli, hofu yake ya watu hao ilikuwa ni kuu mno, hivi kwamba akamwendea nabii wa kukodisha aliyeitwa Balaamu na akamwomba awe mpatanishi kati yake na Mungu na amsihi Mwenyezi awalaani Israeli, na azivunje nguvu zao kabisa. Basi Balaamu, akiwa na shauku ya kushiriki katika mambo ya kisiasa na kuwa mtu mkuu, alifurahia tu sana kufanya hivyo. Lakini alipoona ya kwamba ilimlazimu amkaribie pia, asikilizwe na Mungu kusudi hao watu wapate kulaaniwa kwa kuwa hangeweza kufanya hivyo yeye mwenyewe, akaenda kumwuliza Mungu kama angeweza kumpa ruhusa aende. Sasa je! jambo hilo silo kama tu Wanikolai tulio nao siku hizi? Wao hulaani ye yote ambaye hangefuata njia zao.

Wakati Balaamu alipomwomba Mungu ruhusa ya kwenda, Mungu alimkatalia. Jamani liliuma! Lakini Balaki alisisitiza, akimwahidi hata zawadi kubwa zaidi na heshima. Kwa hiyo Balaamu akarudi kwa Mungu. Sasa jibu moja toka kwa Mungu lingetosha. Lakini sio kwa Balaam mkaidi. Mungu alipoona ukaidi wake, alimwambia asimame aende. Upesi akamtandika punda akaondoka akaenda zake. Yeye angepaswa kutambua ya kwamba haya yalikuwa tu mapenzi ya Mungu ya kuruhusu naye asingaliweza kuwalaani hata kama angeenda mara ishirini na kujaribu mara ishirini. Jinsi watu siku hizi walivyo kama Balaamu! Wanaamini katika Miungu mitatu, wanabatizwa katika vyeo vitatu badala ya JINA, na hata hivyo Mungu atamtuma Roho juu yao kama vile alivyofanya juu ya Balaamu, nao wataendelea kuamini kuwa wao wako sahihi kabisa, nao ndio hawa hapa akina Balaamu kwa kweli kabisa. Mnaona, fundisho la Balaamu. Endelea hata hivyo. Fanya upendavyo. Wao husema, "Naam, Mungu ametubariki. Lazima liwe ni sahihi." Ninajua Yeye amewabariki. Sikatai hilo. Lakini ni njia ile ile ya kimadhehebu ambayo Balaamu alipitia. Ni ya kuasi Neno la Mungu. Ni fundisho la uongo.

Kwa hiyo Balaamu alishuka akaenda barabarani kwa ukaidi mpaka malaika aliyetoka kwa Mungu akasimama mbele zake. Lakini huyo nabii (askofu, kadinali, mwenye kiti, rais na msimamizi mkuu) alipofushwa mno katika mambo ya Kiroho kwa wazo la heshima na utukufu na pesa hata hakuweza kumwona malaika mwenye upanga uliochomolewa amesimama. Huyo hapo amesimama amzuie nabii mwenye kichaa. Maskini yule punda alimwona na akakwepa kwa nyuma na mbele hadi mwishowe akamseta Balaamu mguu wake kwenye ukuta wa mawe. Yule punda akasimama na hangeendelea kwenda. Hangeweza kwenda. Kwa hiyo Balaamu akaruka na kuanza kumpiga. Yule punda akaanza kuzungumza na Balaamu. Mungu alimwacha punda huyo anene kwa lugha. Punda huyo hakuwa chotara; yeye alikuwa ni mbegu asili. Akamwambia nabii aliyepofushwa, "Je! mimi si punda wako, nami, je! sijakubeba wewe kwa uaminifu?" Balaamu akamjibu, "Ndiyo, ndiyo, wewe u punda wangu nawe umenibeba kwa uaminifu hadi sasa; na ikiwa siwezi kukufanya utembee, nitakuua..." masalale! ni kitu gani hiki, kuzungumza na punda? Ajabu hii, nadhani nilimsikia huyu punda akizungumza nami nilikuwa nikimjibu."

Mungu daima amenena kwa lugha. Yeye alinena kwenye karamu ya Belshaza kisha kwenye Pentekoste. Yeye anafanya hivyo tena leo. Ni onyo la hukumu ijayo.

Ndipo yule malaika akaonekana na Balaamu. Naye akamwambia Balaamu kama si punda yeye angekuwa amekufa hata sasa hakika kwa kumjaribu Mungu. Lakini Balaamu alipoahidi kurudi, alitumwa aende na onyo la kusema yale tu Mungu aliyompa.

Kwa hiyo Balaamu akashuka akaenda akatengeneza madhabahu saba kwa ajili ya wanyama safi wa sadaka. Akachinja kondoo dume kuonyesha kuja kwa Masihi. Alijua la kufanya apate kumkaribia Mungu. Mitambo yake ilikuwa sawa; bali si nguvu za kuendesha; ndivyo iliyvo sasa. Hivi hamwezi kuona enyi Wanikolai? Kule chini bondeni walikuweko Israeli wakitoa dhabihu ile ile, wakifanya mambo yale yale lakini ni mmoja tu aliyekuwa na ishara zilizofuata. Ni mmoja tu aliyekuwa na Mungu kati yao. Desturi hazitakufikisha po pote. Haziwezi kupachukua mahali pa dhihirisho la Roho. Jambo hilo ndilo lililotukia kule Nikea. Waliyachukua mafundisho ya Balaamu, si mafundisho ya Mungu. Nao wakajikwaa; naam walianguka. Wakawa watu waliokufa.

Baada ya dhabihu kutolewa, Balaamu alikuwa tayari kutabiri. Lakini Mungu akaufunga ulimi wake naye hakuweza kuwalaani. Aliwabariki.

Balaki alikasirika sana, lakini hapakuwepo na chochote ambacho Balaamu angeweza kufanya kuhusu huo unabii. Ulikuwa umenenwa na Roho Mtakatifu. Kwa hiyo Balaki akamwambia Balaamu ashuke chini,

aende katika lile bonde, akaangalie upande wao wa nyuma aone kama kuna uwezekano wa kuweza kuwalaani kwa njia fulani. Mbinu alizotumia Balaki ni zile zile wanazotumia leo. Madhehebu makubwa hudharau vikundi vidogo, na cho chote wanachopata kati yao kiwezacho kusababisha kashifa wao wanakichukua na kukitangaza. Kama watu wa kisasa wakiishi katika dhambi, hakuna mtu anayesema neno juu yake; bali hebu mmoja wa wateule apatikane na shida na kila gazeti litalilipua kote nchini. Naam, Israeli alikuwa na sehemu zake dhaifu (kimwili). Walikuwa na upande wao usio mwema; bali licha ya kutokamilika kwao, kwa kusudi la Mungu ambalo hufanya kazi kwa uchaguzi, kwa neema wala si kwa matendo, WALIKUWA NA WINGU MCHANA NA NGUZO YA MOTO USIKU, WALIKUWA NA MWAMBA ULIOPIGWA, NYOKA WA SHABA NA ISHARA NA MAAJABU. Walithibitishwa—si kwa juhudi zao, bali katika Mungu.

Mungu hakuwatakabali wale Wanikolai na PHD zao, LLD na DD zao na madhehebu yao yote mazuri na mambo bora sana ambayo mwanadamu angejivunia; bali Yeye aliwatakabali Israeli kwa kuwa walikuwa na Neno lililothibitishwa kati yao. Hakika Israeli hawakuonekana wameadibika sana, wakiwa tu ndio kwanza watoke Misri kwa kutoka mbio mbio, lakini walikuwa watu waliobarikiwa haidhuru. Yote walichokuwa wamewahi kujua kwa zaidi ya miaka 300 ilikuwa ni kuchunga kondoo, kulima mashamba na kufanya kazi ya utumwa huku wakiwa na hofu ya kifo chini ya Wamisri. Lakini walikuwa huru sasa. Walikuwa watu waliobarikiwa kwa mamlaka ya Mungu. Bila shaka Moabu waliwadharau. Mataifa mengine yote yalifanya hivyo, pia. Madhehebu daima huwadharau wasio na madhehebu na aidha watawashurutisha wajiunge na madhehebu la sivyo watawaangamiza wasipokuja.

Basi huenda mtu angeniuliza, "Ndugu Branham, ni kitu gani kinachokufanya ufikirie kuwa Moabu walikuwa wa kimadhehebu ambapo Israeli hawakuwa hivyo? Unalipata wapi wazo hilo?" Ninalipata papa hapa katika Biblia. Lote limeonyeshwa hapa katika mfano. Kila kilichoandikwa katika Agano la Kale kilicho katika namna ya hadithi kimaandikwa kwa ajili ya kutuonya ili tuweze kujifunza kwa hilo.

Hili hapa papa hapa katika Hesabu 23:9,

> *"Kutoka kilele cha majabali namwona, na kutoka milimani namtazama; angalia, ni watu wakaao PEKE YAO, wala HAWATAHESABIWA PAMOJA NA MATAIFA."*

Hilo hapo. Mungu akiangalia chini kutoka kwenye kilele cha majabali, si kutoka kwenye bonde fulani akiyaangalia mabaya yao na kuwahukumu. Mungu akiwaona jinsi alivyotaka kuwaona_kutoka kwenye kilele cha upendo na rehema. Waliishi PEKE YAO na hawakuwa na madhehebu. Hawakuwa na mfalme. Walikuwa na nabii, naye nabii alikuwa na Mungu ndani yake kwa Roho; nalo Neno lilimjia nabii na hilo Neno likawaendea watu. Hawakuwa washiriki wa Umoja wa Mataifa. Hawakuwa wa Baraza la Makanisa Ulimwenguni, wala wa Wabatisti, wa Wapresbiteri, wa Asemble of God wala kundi jingine lo lote. Hawakuwa na haja ya kuwa wa kundi fulani. Walikuwa wameunganishwa na Mungu. Hawakuhitaji shauri kutoka kwa halmashauri yo yote_walikuwa na "Bwana asema hivi" kati yao. Haleluya!

Basi licha ya ukweli kwamba Balaamu alijua njia iliyo sawa ya kukutana na Mungu na angeweza kuleta ufunuo toka kwa Bwana kwa njia maalumu ya nguvu ya kipawa, yeye alikuwa angali bado licha ya hayo yote askofu katika kundi la uongo. Kwa kuwa alifanya nini sasa ili apate kujipendekeza kwa Balaki? Alibuni mpango ambapo Mungu angelazimika kumwua Israeli. Kama tu vile Shetani alivyojua kuwa angeweza kumdanganya Hawa (kumfanya aanguke kwa dhambi ya kimwili) na hivyo basi akamfanya Mungu amhukumu kwa hukumu Yake aliyoitangaza ya kifo dhidi ya dhambi, vivyo hivyo Balaamu alijua ya kwamba kama angeweza kuwafanya Israeli watende dhambi, Mungu angewaua. Kwa hiyo yeye alipanga njia ya kuwanasa wao waje kushiriki katika dhambi. Alipeleka mialiko kuja kwenye karamu ya Baal-Peori (mje huku na mwabudu nasi). Basi Israeli, bila shaka, walikuwa wameona karamu za Wamisri kwa hiyo hawakuona kuwa ilikuwa ni vibaya sana kwenda na kuangalia tu na pengine kula pamoja na watu wale. (Kuna ubaya gani kwani kuwa na ushirika? Tunapaswa kuwapenda sivyo? au tutawezaje kuwavuta?) Kufanya urafiki hakumdhuru ye yote_ama ndivyo walidhania. Lakini wakati wale wanawake wazinzi wa Moabu walipoanza kucheza na kuvua nguo wakati walipokuwa wanajizungusha wakicheza rumba zao na kukata viuno, tamaa iliwaka miongoni mwa Waisraeli nao wakazini ndipo Mungu kwa ghadhabu akawaua elfu arobaini na mbili kati yao.

Na hivyo ndivyo Konstantino na waliomfuata walivyofanya huko Nikea na baada ya Nikea. Waliwaalika watu wa Mungu kwenye mkutano. Na kanisa lilipokaa chini kula, kisha likaamka kucheza (likishiriki katika desturi za kanisa, ibada, na karamu za kipagani zilizopewa majina ya ibada za Kikristo), lilinaswa; lilifanya uzinzi. Ndipo Mungu akaondoka.

Wakati mtu ye yote anapoliacha Neno la Mungu na kujiunga na kanisa badala ya kumpokea Roho Mtakatifu, mtu huyo anakufa. Amekufa! Hivyo ndivyo alivyo. Usijiunge na kanisa. Usiingie katika madhehebu na kuchukuliwa na kanuni za imani na mapokeo au kitu cho chote ambacho hupachukua mahali pa Neno na Roho, la sivyo umekufa. Imekwisha. Umekufa. Umetengwa milele na Mungu!

Hilo ndilo lililotukia katika kila wakati tangu wakati huo. Mungu huwakomboa watu. Wanatoka kwa njia ya damu, wakiwa wametakaswa kwa Neno, na kupitia katika maji ya ubatizo na kujazwa na Roho; lakini

baada ya muda mfupi upendo wa kwanza unapoa halafu mtu fulani anapata wazo kwamba yawapasa waunde madhehebu ili wajinusuru na kujitengenezea jina, basi wanaunda madhehebu moja kwa moja tena katika kizazi cha pili na pengine hata kabla ya hapo. Hawana Roho wa Mungu tena, ni namna tu ya kuabudu. Wamekufa. Wamejichanganya na kanuni za imani na desturi na hamna uhai ndani yao.

Kwa hiyo Balaamu akawafanya Israeli wafanye uzinzi. Je! wajua uasherati wa kimwili ni roho yule yule ambaye hukaa katika madhehebu ya dini? Nilisema ya kwamba roho ya uasherati ni roho ya madhehebu. Na wazinzi wote watapata mahali pao katika lile ziwa la moto. Hivyo ndivyo Mungu anavyowazia juu ya madhehebu. Naam bwana, yule kahaba na binti zake watakuwa katika ziwa la moto.

Madhehebu si ya Mungu. Hawajawahi kuwa na wala hawatakuwa. Ni roho mbaya anayewatenganisha watu wa Mungu katika madaraja ya makasisi na washiriki; na kwa hiyo, basi, ni roho mbaya anayebagua watu na watu. Hivyo ndivyo shirika na madhehebu yafanyavyo. Katika kujiundia madhehebu wao hujitenga na Neno la Mungu, na kujiingiza katika uzinzi wa kiroho.

Sasa tazama ya kwamba Konstantino aliwapa watu karamu maalum. Zilikuwa ni zile karamu za kipagani za kale zikiwa na majina mapya yaliyotolewa katika kanisa, au wakati mwingine ibada za Kikristo zilichukuliwa na kutumiwa isivyo katika ibada za kipagani. Alichukua ibada ya mungu jua na kuibadilisha kuwa ya Mwana wa Mungu. Badala ya kuiadhimisha mnamo tarehe 21 Desemba, ambayo ndiyo walipokuwa wakisherehekea karamu ya mungu jua, waliiweka iwe Desemba 25 na kuiita siku ya kuzaliwa kwa Mwana wa Mungu. Bali tunajua kuwa alizaliwa Aprili wakati ambapo uhai unatokeza, si Desemba. Nao wakazichukua karamu za Astarte na kuziita shehere za Pasaka ambayo kwayo Mkristo anapaswa kuadhimisha kifo na kufufuka kwa Bwana. Kwa kweli hiyo ilikuwa ni karamu ya kipagani ya Astarte.

Waliweka madhabahu kanisani. Waliweka sanamu. Waliwapa watu kile walichokiita imani ya mitume, ingawa huwezi kuipata katika Biblia. Waliwafundisha watu kuabudu mizimu hivyo basi linalifanya Kanisa Katoliki la Kirumi kuwa kanisa kuu kuliko yote yanayoabudu mizimu ulimwenguni. Kila ndege mchafu alikuwa katika kizimba hicho. Na kuna Waprotestanti nao na madhehebu yao wanaofanya mambo yale yale.

*Walikula vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu.* Sasa sisemi ya kwamba hili hasa lina maana kwamba walikuwa wakila kweli vyakula vilivyotolewa sadaka kwa sanamu. Kwa maana ingawa mkutano wa Yerusalemu ulikataza vitu kama hivyo, Paulo hakulititilia jambo hilo mkazo sana kwa kuwa alisema sanamu sio kitu. Ilikuwa tu ni jambo la dhamiri isipokuwa pale tu ambapo lilimkwanza ndugu aliyezidi kuwa mnyonge na ndipo basi halikukubaliwa. Isitoshe, Ufunuo huu unawahusu Mataifa wala si Wayahudi kwa kuwa haya ni makanisa ya Mataifa. Ninaliona jambo hili katika nuru ile ile ninavyoyaona maneno ya Bwana, "Msipoula mwili Wangu na kuinywa damu Yangu hamna uzima ndani yenu. Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Waweza kuona kuwa kula kwa hakika ni kushiriki katika hali ya kiroho.

Kwa hiyo wakati hawa watu walipokuwa wakisujudia sanamu, wakiwasha mishumaa, wakitumia sikukuu za kipagani, wakiziungama dhambi zao kwa wanadamu (ambayo yote ni dini ya ibilisi), walikuwa wakishirikiana na ibilisi wala sio Bwana. Walikuwa katika ibada ya sanamu wakubali wasikubali. Wanaweza kusema yote watakayo kwamba madhabahu na uvumba ni kuwakumbusha tu maombi ya Bwana au lo lote wanalodhani hayo yanamaanisha; nao wanaweza kusema kuwa wanapoomba mbele ya sanamu ni kwa kutilia mkazo tu; na kwamba wanapoungama kwa kasisi, eti wanafanya hivyo hasa kwa Mungu ndani ya mioyo yao, nao wanaposema kwamba kasisi anawasamehe, ni kwamba tu anafanya hivyo katika Jina la Bwana; wanaweza kusema watakacho lakini wao wanashiriki katika dini inayojulikana sana ya Babeli na ya Shetani, nao wamejiunga na sanamu na wametenda uasherati wa kiroho, ambao maana yake ni mauti. Wamekufa.

Kwa hiyo kanisa lilifunga ndoa na serikali. Kanisa lilijiunga na sanamu. Huku wakisaidiwa na nguvu za serikali walijisikia kuwa sasa, "Ufalme umekuja na mapenzi ya Mungu yameingizwa kwa nguvu duniani." Si ajabu Kanisa la Katoliki la Kirumi halitarajii kurudi kwa Bwana Yesu. Wao hawaamini katika ule utawala wa miaka elfu. Wao wana utawala wao wa miaka elfu papa hapa. Papa anatawala hivi sasa na Mungu anatawala ndani yake. Kwa hiyo Yeye atakapokuja kulingana nao, haina budi kuwa ni wakati ambapo mbingu mpya na nchi mpya zinaandaliwa. Lakini wamekosea. Papa ni kiongozi wa kanisa la uongo, na kutakuwako na ule utawala wa miaka elfu, ila wakati huo unapoendelea yeye hatakuwamo. Atakuwa mahali pengine.

**ONYO**

Ufunuo 2:16.

> *"Basi tubu, na usipotubu, Naja kwako upesi, Nami nitafanya vita juu yao kwa huo upanga wa kinywa Changu."*

Anaweza kusema nini kingine? Hivi Mungu aweza kuachilia dhambi za hao ambao wamelichukua Jina

Lake bure? Pana njia moja tu ya kupokea neema katika wakati wa dhambi, TUBU. Ungama umekosea. Njoo kwa Mungu kwa msamaha na kwa Roho wa Mungu. Hii ni amri kutoka kwa Mungu. Kutotii ni mauti, kwa kuwa Yeye anasema, "Nitafanya vita nanyi kwa upanga kinywani Mwangu." Yule mnyama alifanya vita na watakatifu, bali Mungu atafanya vita na yule mnyama. Wale waliolipiga Neno siku moja wataliona Neno likipigana nao. Ni jambo zito kuondoa, au kuongeza kwenye Neno la Mungu. Kwa maana wale waliolibadilisha, na wakafanya nalo walivyotaka, mwisho wao utakuwa nini ila mauti na maangamizi? Bali bado neema ya Mungu inapaza sauti, "Tubu." Loo! jinsi mawazo ya toba yalivyo matamu. Sina kitu mkononi ninachokuletea, nashikilia tu kwenye msalaba Wako. Ninaleta huzuni yangu. Natubu ya kwamba mimi niko jinsi nilivyo, na yale niliyofanya. Sasa ni damu, si kitu ila damu ya Yesu. Itakuwaje? Kutubu, ama upanga wa mauti? Ni juu yako.

**THAWABU**

Ufunuo 2:17

*"Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa. Yeye ashindaye nitampa baadhi ya ile mana iliyofichwa, nami nitampa jiwe jeupe, na juu ya jiwe hilo limeandikwa jina jipya asilolijua mtu ila yeye anayelipokea."*

Kila ujumbe kwa kila wakati una kitu cha kumtia moyo mwamini, kumpa moyo awe mshindi na hapo atunukiwe na Bwana. Katika wakati huu Roho anaahidi mana iliyofichwa na jina jipya lililoandikwa ndani ya jiwe jeupe.

Sasa kwa kuwa kila mmoja wa jumbe hizi umeelekezwa kwa „malaika"_(mjumbe wa kibinadamu) wajibu mkubwa sana na pia majaliwa makuu sana ni fungu lake. Mungu anatoa ahadi maalum kwa watu hawa, kama vile ilivyo kwa wale mitume kumi na wawili kuketi kwenye viti kumi na viwili vya enzi wakiwahukumu makabila kumi na mawili ya Israeli. Basi, kumbuka Paulo alipewa ahadi maalum: ile ya kumkabidhi Yesu watu wa bibi-arusi wa siku yake,

II Wakorintho 11:2

*"Maana nawaonea wivu, wivu wa Mungu; kwa kuwa naliwaposea mume mmoja, ili nimletee Kristo bikira safi."*

Ndivyo itakavyokuwa kwa kila mjumbe ambaye amekuwa mwaminifu kwa Neno la saa yake na kipindi cha wakati wake. Itakuwa hivyo katika siku ya mwisho. Itakuwa thawabu ile ile maalum aliyopewa Paulo. Nafikiri karibu ninyi nyote mnakumbuka jinsi nilivyosema daima niliogopa kufa nisije nikakutana na Bwana Naye asipendezwe nami kwa kuwa nilikuwa nimekosea mara nyingi sana. Vema, nilikuwa nikiwazia jambo hili asubuhi moja wakati nilipokuwa mimelala kitandani na mara nikanyakuliwa katika ono la ajabu sana. Ninasema lilikuwa la ajabu kwa kuwa nilikwishapata maelfu ya maono wala hakuna wakati hata mmoja ni nilionekana ninauacha mwili wangu. Lakini nilikuwa mimi hapo nimenyakuliwa; nami nikaangalia nyuma kumwona mke wangu, nami nikaona mwili wangu umelala pale kando yake. Ndipo nikajikuta katika mahali pazuri mno nilipopata kuona. Ilikuwa ni paradiso. Nikaona msongamano wa watu wenye sura nzuri sana na wenye furaha sana niliopata kuona. Wote walionekana ni vijana sana—yapata umri wa miaka 18 hadi 21. Hapakuwa na unywele wa mvi wala kunyazi lo lote wala kilema cho chote miongoni mwao. Vijana wanawake wote walikuwa na nywele zilizofika viunoni mwao, na vijana wanaume walikuwa wenye sura nzuri sana na wenye nguvu. Loo, jinsi walivyonikaribisha. Walinikumbatia na kuniita ndugu yao mpenzi, na kuendelea kuniambia jinsi walivyokuwa na furaha kuniona. Nilipokuwa nikishangaa umati wote huo ni akina nani, mmoja aliyekuwa karibu nami akasema, "Hao ni watu wako."

Nilishangaa sana nikauliza, "Hawa wote ni Wabranham?"

Akasema, "La, hao ndio waongofu wako." Ndipo akaelekeza kidole kwa bibi mmoja na kusema, "Unamwona yule bibi kijana uliyekuwa ukimshangaa sana muda kidogo uliopita. Alikuwa na umri wa miaka 90 wakati ulipomleta kwa Bwana."

Nikasema, "Loo jamani, na hebu wazia jambo hili ndilo nililokuwa nikiogopa."

Huyo mtu akasema, "Tunapumzika hapa huku tukingojea kuja kwa Bwana."

Nikajibu, "Ninataka kumwona Yeye."

Akasema, "Huwezi kumwona sasa; lakini yuaja upesi, na wakati atakapokuja atakuja kwako kwanza, nawe utahukumiwa kulingana na Injili uliyohubiri, nasi tutakuwa raia wako."

Nikasema, "Una maana kwamba ninawajibika kwa hawa wote?"

Yeye alisema, "Kila mmoja. Ulizaliwa ukiwa kiongozi."

Nilimwuliza, "Je, kila mmoja atawajibika? Vipi kuhusu Mtakatifu Paulo?"

Akanijibu, "Atahusika na siku yake."

"Vema," nikasema, "Nimehubiri Injili ile ile aliyohubiri Paulo." Na makutano wakapaza sauti, "Tunategemea jambo hilo."

Naam, ninaweza kuona ya kwamba Mungu atatoa thawabu maalum kwa wajumbe Wake ambao wamekuwa waaminifu katika kutekeleza wajibu ambao Yeye ameweka juu yao. Kama wao wamepokea ufunuo wa Neno kwa ajili ya wakati huo na kulihubiri kwa uaminifu katika siku yao, na kuishi yale waliyohubiri, watapokea thawabu kuu.

Sasa tukiwa na wazo hili moyoni, tazama aya hiyo tena. "Nitampa mana iliyofichwa." Sote tunajua ya kwamba mana hiyo ilikuwa ni chakula cha malaika; ilikuwa ni kile Mungu alichoshusha chini juu ya nyasi kwa ajili ya Israeli wakati wa kuzungukazunguka kwao. Kilikuwa ni chakula kikamilifu. Ilikuwa ni kitu cha kustaajabisha sana jinsi vidonge hivyo vidogo vya chakula vilivyowaweka katika afya kamilifu. Hakuna mtu aliyeugua. Ilikuwa tu ndiyo waliyohitaji. Wakati lile sanduku lilipotengenezwa waliweka baadhi ya mana hiyo humo ndani. Kisha sanduku hilo likawekwa nyuma ya pazia na ni kuhani mkuu tu ndiye angethubutu kulikaribia na halafu ilimbidi kuwa na damu ya sadaka. Chakula kitokacho mbinguni, kilichowakilishwa na mana, siku moja kilishuka kutoka mbinguni na kikawa Uzima kwa wote wanaomwamini Yeye. Yeye alisema, "Mimi ndimi chakula cha uzima. Mimi ni chakula kilicho hai kilichoshuka kutoka mbinguni, mtu ye yote akila chakula hiki ataishi milele." Wakati alipoondoka Yeye alituachia Neno Lake, "Mtu hataishi kwa mkate tu bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

Neno Lake lilikuwa mkate. Ilikuwa ni mana kamilifu, ambayo, mtu akiishi kwayo, hatakufa kamwe. Lakini mara baada ya kufa kwa wale waanzilishi, hakuna mtu aliyeonekana anajua ile kweli halisi na haikupita muda mana hii ilionekana imefichwa kwa watu. Lakini katika kila wakati Mungu alianza kurudisha kwa ufunuo kile ambacho kilikuwa kimefichwa hata siku hii ya mwisho kulingana na Ufu. 10:7, nabii atakuja na kufunua siri zote halafu Bwana atakuja. Sasa katika kila wakati, nasema, wale wajumbe walipokea ile kweli iliyofichwa. Lakini hawakuipokea kwa ajili yao tu. Lakini ni kama ilivyokuwa wakati wale wanafunzi walipoambiwa wawahudumie yale makutano mikate na samaki; Yesu aliwapa chakula kilichovunjwavunjwa, lakini wao nao wakawapa watu tena. Mungu humpa mwenye kushinda mana yake iliyofichwa. Haiwezi kuwa vinginevyo. Asingeweza kufungua hazina Zake kwa wale wanaokataa yale yaliyofunuliwa tayari.

Yale niliyokuwa nikisema juu ya mjumbe wa kila wakati akipokea kutoka kwa Mungu sehemu ya ile kweli ya asili ya Pentekoste yanaonyeshwa kwa mfano katika Agano la Kale ambapo Musa aliamriwa kuchukua painti tatu na nusu za mana na kuiweka katika chombo cha dhahabu nyuma ya pazia la patakatifu pa patakatifu. Hapo kuhani mkuu wa kila kizazi angeweza kuingia akiwa na damu ya dhabihu. Ndipo angechukua sehemu kidogo ya mana hii (kwa kuwa haikuoza) ambayo ilikuwa sehemu ya ile ya asili na kuila. Sasa katika kila wakati mjumbe wa Bwana kwa kipindi cha wakati huo alipewa ufunuo wa Mungu kwa ajili ya kipindi hicho hicho. Mara mjumbe huyo alipoangaziwa na ile kweli, angeileta hiyo kweli kwa watu. Na hao ambao maskio yao yalikuwa yamefunguliwa na Roho wangeisikia hiyo kweli, wakaiamini, na kuiishi.

Sasa basi, kuna wazo pia la kula ile mana iliyofichwa katika siku zijazo. Nafikiri itakuwa kula kwa milele kwa ufunuo wa Yesu Kristo katika nyakati za milele zijazo. Tungewezaje basi kuanza kujua utajiri usiopimika wa Utu Wake? Yote ambayo tumetamani kujua, maswali yetu yote ambayo hayajajibika, yote hayo yatafunuliwa. Tutaupokea kutoka kwa Kristo Ambaye kwamba Ndiye uzima wetu. Loo! wakati mwingine tunafikiri tunafahamu kidogo juu yake na Neno Lake hapa chini, na ni jambo zuri sana, linatufanya tushangilie; lakini siku moja wakati miili yetu itakapobadilika, Neno hilo pamoja na Yeye watakuwa jinsi ambavyo hatujawazia inawezekana.

Pia inasemwa hapa ya kwamba Yeye atampa mwenye kushinda jiwe jeupe na ndani ya (si juu ya) jiwe hilo jina jipya, ambalo linajulikana tu na huyo mwenyewe. Sasa wazo la jina jipya linajulikana. Abramu alibadilishwa akawa Ibrahimu, Sarai akawa Sara, Yakobo akawa Israeli, Simoni akawa Petro, na Sauli akawa Paulo. Majina haya aidha yalisababisha badiliko, ama yalitolewa kwa sababu ya badiliko. Ilikuwa tu ni baada ya Abramu na Sarai kubadilishwa majina na Bwana ndipo walipotayarishwa kumpokea yule mwana ajaye. Katika kisa cha Yakobo, ilimbidi kushinda na ndipo akaitwa mtawala. Kuhusu Simoni na Sauli, walipokwisha kumpokea Bwana, badiliko lao likaja. Na hivi leo kila mmoja wetu sisi waamini wa kweli amekuwa na badiliko la jina. Sisi ni Wakristo. Ni jina la kawaida kwetu sote. Lakini siku moja tutapata badiliko lingine; bila shaka tutapokea jina jipya. Huenda ikawa jina hilo lilikuwa ndilo jina letu la kweli na la asili lililoandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Yeye analijua jina hilo, lakini sisi atulijui. Siku moja kwenye uradhi wa mapenzi Yake, sisi nasi tutajua pia.

Jiwe jeupe. Ni jambo zuri jinsi gani. Hii hapa picha nyingine ya mtakatifu akipokea tuzo kutoka kwenye mkono wa Mungu kwa ajili ya majaribu yake duniani. Unajua, baada ya Konstantino, lile kanisa la uongo liliweza kuingiza mkono wake katika hazina ya serikali na hivyo kujenga majengo mazuri yaliyojaa sanamu za kuchonga zenye kupendeza. Sanamu hizi za kuchonga, zilizotengenezwa kwa marumaru

nyeupe, kwa kweli zilikuwa ni sanamu za Kirumi zilizopewa majina mapya ya watakatifu. Hayo makanisa na mapambo yake yalikuwa ni mazuri kupita kiasi, kama vile mtu anavyoyaona leo hii. Lakini Mungu hakuwa pamoja nao. Mungu alikuwa wapi? Alikuwa pamoja na watakatifu Wake katika makao fulani madogo, ama katika pango, ama kwenye sehemu fulani ya mlima msituni ambako walijificha wasionekane na wafuasi wa kanisa la uongo. Wao hawakuwa na majengo mazuri ya kuvutia, kwaya zilizovikwa majoho, nguo nzuri, na vivutio vingine vya kilimwengu. Lakini sasa katika ahadi hii maalum kwa waamini wa kweli wa nyakati zote, Mungu ametangaza Yeye atawapa thawabu zenye uzuri mkuu na udumuo milele. Acha matajiri wawadharau maskini. Acha watoe kiasi kikubwa cha fedha kwa kanisa ili nalo liweze kumheshimu huyo mfadhili kwa kuweka kipande chembamba cha marumaru ama sanamu fulani ya kuchonga kwa heshima yao ili watu wote wapate kukiona na kuwashangilia. Siku moja Mungu Ambaye anaona na kujua yote mara nyingine tena atamsifu mjane kwa kutoa yote aliyo nayo, ingawa yaweza kuwa ni senti mbili tu, Naye, Yeye Mwenyewe, atawapa thawabu za hazina ya mbinguni.

Naam, mana iliyofichwa na jina jipya ndani ya jiwe jeupe. Jinsi Bwana alivyo mwema kwetu kututunukia vizuri hivi, nasi tukiwa hatustahili kabisa. Loo, nataka kuwa tayari wakati wote kufanya mapenzi Yake, na kuweka hazina mbinguni.

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7